BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TANO

Kikao cha Kumi – Tarehe 11 Novemba, 2016

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge tukae.

Katibu!

NDG. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:

TAARIFA YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa masikitiko makubwa nawatangazia msiba tuliopata wa mwenzetu Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani Zanzibar kupitia Chama cha Mapinduzi, msiba uliotokea saa nane kamili usiku wa kuamkia leo katika Hospitali ya *General* hapa Dodoma.

Marehemu Hafidh Ali Tahir aliugua kwa muda mfupi ambapo baada ya kujisikia vibaya aliamua kwenda hospitali mwenyewe usiku wa jana na alipofika alikutwa na tatizo la moyo na akiwa katika matibabu alifariki.

Ni masikitiko makubwa kwa sababu ni jana tu mimi nilikuwa naye katika Kikao cha Bunge *Sports Club* na pia alishughulika katika semina mbalimbali za Wabunge zilizofanyika Dodoma *Hotel* na hapa Bungeni na pia baadhi yetu tulikuwa naye katika kikao cha Bunge humu ndani na tulifanya kazi vizuri sana kwa pamoja.

Vile vile Marehemu Hafidh Ali Tahir alikuwa ni mmoja wa Wabunge walioomba kwenda Urambo kwenye maziko ya Mheshimiwa Mzee Samuel Sitta, Spika Mstaafu wa Bunge la Tisa na alikuwemo katika orodha ya Wabunge ambao walihitajika kwenda kushiriki katika msiba huo.

Tumeondokewa na Mbunge mchapa kazi, mcheshi, mwanamichezo na pia Mbunge aliowajali sana wapiga kura wake.

Waheshimiwa Wabunge, kwa mujibu wa Kanuni zetu za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016; Kanuni ya 152 kuhusu utaratibu baada ya kifo cha Mbunge inasema na hapa nanukuu:

"Endapo Mbunge atafariki wakati Bunge likiwa katika shughuli zake, Spika ataahirisha shughuli za Bunge kwa siku hiyo kwa ajili ya maombolezo.

Hata hivyo kwa siku ya leo tuna kikao maalum cha kumuaga Marehemu Mzee Samuel Sitta, Spika Mstaafu wa Bunge la Tisa, shughuli ambayo haiwezi kuahirishwa. Hivyo Waheshimiwa Wabunge nitawaomba sana ushirikiano wenu kwa siku ya leo, ili tuendelee na shughuli mbalimbali kwa kadri ya utaratibu nitakaokuwa nimeupendekeza muda si mrefu.

Napendekeza kwamba, muda si mrefu nitamwita Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu au Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kutoa hoja ya kutengua kanuni hiyo ya 152 ili tuweze kuendelea na shughuli za leo hususan kikao maalum cha kumuaga Marehemu Mzee Sitta, pamoja na shughuli za kumwaga Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir ambazo zitatangulia kabla ya hizo za Mzee Sitta ambazo zitafanyika mchana wa leo.

Mtakumbuka Waheshimiwa Wabunge kwamba, jana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Sheria Ndogo aliwasilisha kwamba, Bunge lipokee na kukubali taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo, kuhusu uchambuzi wa sheria ndogo pamoja na maoni na mapendekezo yaliyomo katika taarifa hiyo.

Kwa hoja hiyo, sasa tutamwomba kwa dakika chache sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo, ahitimishe bila mjadala ili tuweze kuikabidhi Serikali ifanyie kazi taarifa hiyo.

Baada ya hapo kwa shughuli hizo ndogo sana zitakazofanyika asubuhi hii ya leo tutawapa utaratibu, nitaueleza baadaye kidogo jinsi tutakavyotoka hapo nje na kutekeleza utaratibu wa kumpa heshima za mwisho ndugu yetu, mwenzetu Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir.

Kwa hiyo mchana tutakapokuwa tumeshamaliza shughuli ya kumuaga Mzee Sitta itatolewa hoja ya kuahirisha Bunge na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kifupi sana, kinyume na tulivyozoea. Kwa hiyo atakachofanya Mheshimiwa Waziri Mkuu ni kutoa tu hoja bila hotuba.

Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge, muda si mrefu nitasitisha shughuli za Bunge za leo hapa asubuhi mpaka saa 8.40 mchana ambapo tutaendelea na zile shughuli nilizosema za utaratibu wa kumuaga Mzee Sitta.

Sasa kabla sijasitisha shughuli za mchana huu na kwa ridhaa yenu, naomba Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu atoe hoja ya kutengua ile Kanuni ya 152. Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

HOJA YA KUTENGUA KANUNI

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WATU WENYE WALEMAVU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi katika siku hii ambayo ni nzito sana kwa Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa heshima yako na maelezo yako ya utangulizi nitoe hoja ya kutengua Kanuni za Bunge kama ifuatavyo:-

KWA KUWA Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania limepatwa na Msiba wa Mheshimiwa ndugu yetu Hafidh Ali Tahir, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani kule Zanzibar;

NA KWA KUWA chini ya Kanuni ya 152 ya Bunge imeweka utaratibu kuwa endapo Mbunge mwenzetu atafariki wakati Bunge likiwa katika shughuli zake Mheshimiwa Spika ataahirisha shughuli za Bunge kwa siku hiyo kwa ajili ya maombolezo;

NA KWA KUWA katika kikao cha leo imepangwa pia kuwa na kikao maalum cha kutoa heshima za mwisho kwa marehemu Mheshimiwa Samuel John Sitta na baadaye kufuatiwa na hoja ya kuahirisha Bunge;

HIVYO BASI naomba nitoe hoja kwamba Kanuni ya 152 itenguliwe ili Bunge liahirishwe kama Kanuni hiyo inavyoelekeza na badala yake Bunge lisitishwe kwa muda na baadaye kurejea ili kutoa heshima za mwisho kwa mwili wa marehemu Spika Mstaafu Samuel John Sitta na kufuatiwa na hoja ya kuahirisha Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA VIWANDA, BIASHARA NA UWEKEZAJI: Mheshimiwa Spika naafiki.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Naomba Waheshimiwa Wabunge wote tusimame kwa ajili ya kutoa heshima za

mwisho kwa Marehemu Hafidh Ali Tahir na baada ya hapo ndio nitawahoji kuhusiana na hoja iliyotolewa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. Naomba tusimame na kumwombea mwenzetu kimya kimya.

(Hapa Waheshimiwa Wabunge wote walisimama kwa dakika moja)

SPIKA: Tunamwomba Mwenyezi Mungu aipokee na kuiweka mahali pema peponi roho ya marehemu Ndugu yetu, rafiki yetu, kipenzi chetu Hafidh Ali Tahir. Amina.

Sasa hapo hapo mlipo naomba niwahoji. Wale wanaoafiki kuhusiana na hoja iliyotolewa na Mheshimwa Waziri Nchi.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

SPIKA: Wote kabisa wameafiki kwamba twende na utaratibu huo. Naomba Waheshimiwa Wabunge mkae. Kwa hiyo moja kwa moja sasa kwa kifupi kabisa, naomba nimwite Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo, Mheshimiwa Andrew Chenge aje ahitimishe hoja aliyoiwasilisha hapa jana, halafu tutaendelea na maelekezo yanayofuata. Mheshimiwa Chenge tafadhali.

MHE. ANDREW J. CHENGE – MWENYEKITI KAMATI YA SHERIA NDOGO: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipatia fursa hii katika mazingira ambayo sote tunafahamu ni ya majonzi makubwa, lakini yote ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu; mwenzetu kituo chake ndio hicho, ya kwake yamekwisha, yanayofuata hakuna anayefahamu**.**

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, napenda nitumie muda mfupi sana kuhitimisha hoja ambayo niliiwasilisha jana kupitia Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria Ndogo. Nimshukuru sana Mheshimiwa William Ngeleja kwa wasilisho lake zuri, lakini pia naamini pamoja na hali yetu tete hii, tulipata nafasi ya kuipitia kidogo taarifa hiyo pamoja na bangokitita ambalo liliwasilishwa pamoja na taarifa hiyo.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru wewe kwa busara yako ya kuamua kuanzisha Kamati hiyo na isimame bila kuegemea kwa Kamati nyingine kama ilivyokuwa huko nyuma. Uamuzi wako huo ndio uliowezesha kuyaona mengi ambayo yanafanyika kupitia sheria ndogo.

Mheshimiwa Spika, tuendelee kutambua kwamba sheria ndogo ni sheria za nchi na kama tulivyosema kwenye taarifa zinawagusa wananchi wetu katika maisha yao ya siku hadi siku. Pia Bunge linapokasimu madaraka yake kwa

mamlaka nyingine haimaanishi kwamba imejivua majukumu yake na ndiyo maana ya udhibiti na usimamizi. Sheria ndogo hizo zinapowasilishwa na Serikali hapa Mezani lengo ni kuhakikisha kwamba Bunge linazipitia ili lijiridhishe kwamba madaraka iliyokasimu kwa mamlaka nyingine yametumika vizuri.

Mheshimiwa Spika, katika mapendekezo yetu hayo Wabunge kitu kizuri ambacho kimefanyika, maana sisi kama Bunge hatufanyi kazi ya kukinzana na Serikali; Mawaziri walifika mbele ya Kamati na maeneo mengi tulielewana na Serikali, waliona hoja ya Kamati na tukaenda vizuri.

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha hoja hii naomba Bunge hili likubali Serikali ikayafanyie kazi mapendekezo ambayo yamo kwenye taarifa hii kuhusu Sheria ndogo zilizowasilishwa kwenye Mkutano wa Pili, Tatu na Nne; ili sasa watakapokuja kutoa taarifa yao tutajua ni maeneo yapi katika Sheria ndogo yanahitaji kufanyiwa marekebisho.

Mheshimiwa Spika, nikushukuru sana kwa fursa uliyonipatia, niwashukuru sana Wajumbe wa Kamati Ndogo, kwa kazi yao nzuri, iliyotukuka katika kusimamia, kuchambua na kuleta mapendekezo ambayo yameniwezesha leo hii kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

MHE. WILLIAM M. NGELEJA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Andrew Chenge, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Sheria Ndogo. Sasa Waheshimiwa Wabunge napaswa kuwahoji kwamba Serikali ipokee na kuifanyia kazi Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Taarifa ya Kamati ya Sheria Ndogo Kuhusu Uchambuzi wa Sheria Ndogo Ilipitishwa na Bunge)

SPIKA: Wote kabisa wameafiki, kwa hiyo tunaomba sasa Serikali ipokee taarifa hiyo, ipate nafasi ya kuifanyia kazi vizuri, kwa sababu kikao kijacho cha Februari kitakuwa ni kikao ambacho vile vile taarifa mbalimbali za Kamati zitatolewa, nadhani tutapata nafasi ya kujua Serikali imefika wapi kuhusiana na mapendekezo haya yaliyotolewa na Kamati ambayo sasa Bunge linaiomba Serikali iyazingatie

Sasa Waheshimiwa Wabunge, kabla sijasitisha shughuli hizi za asubuhi, kama nilivyosema mwanzoni, mara tu nitakapositisha shughuli, nitawaomba Wajumbe wa Tume ya Huduma za Bunge tukutane kwenye chumba hicho cha Spika, anachovalia joho hapo nje kushoto.

Vilevile nitawaomba Kamati ya Uongozi pamoja na Tume kwa pamoja, tukutane ukumbi wa mikutano wa kawaida wa Spika, saa sita kamili mchana mara tu tukishatoka uwanja wa ndege kumsindikiza Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir. Kutakuwa na baadhi ya wenzetu ambao watatuwakilisha kwenda Zanzibar na kutakuwa na baadhi ya wenzetu watakaotuwakilisha kesho kuelekea Urambo na mipango yote hiyo itapangwa vizuri kuanzia sasa hivi asubuhi na leo mchana kupitia Tume na Kamati ya Uongozi na wale wote ambao mtakuwa mnahusika mtajulishwa namna mbalimbali za ushiriki wa matukio haya mawili makubwa sana.

Siku ya leo imekuwa ni siku nzito sana katika historia ya Bunge letu haijawahi kupata kutokea tukawa na mambo mazito ya kiasi hiki kwa wakati mmoja. Kwa hiyo, pale mtakapoona tumekosea hapa na pale tuchukuliane kwa upendo tu, hakuna aliyedhamiria chochote.

Tukishasitisha shughuli hizi Waheshimiwa Wabunge, nitawaomba sote tutoke nje hapo kwenye korido hapo nje saa tatu na nusu mili wa Marehemu Hafidh Ali Tahir utaletwa pale na tutakuwa na taratibu zitakazoelekezwa pale pale nje tukiwepo ambapo tutamuaga. Tukishamaliza baadhi yetu tutampeleka uwanja wa ndege wa Dodoma, halafu mambo mengine yataendelea kama tulivyosema.

Tukumbuke tu kwamba kuanzia saa 8.30 ni vizuri Waheshimiwa Wabunge muwe mmekaa kwenye viti vyenu leo mchana. Ili tuendelee na ile ratiba nyingine fupi vile vile ya mchana wa leo.

Kwa hatua hiyo, sasa naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa nane na dakika arobaini leo mchana.

(Saa 3.23 Asubuhi Bunge lilisitishwa hadi saa 8.45 Mchana)

(Saa 9.00 Alasiri Bunge lilirudia)

KIKAO MAALUM CHA BUNGE

Kikao Maalum cha Kumuaga Marehemu Mhe. Samuel John Sitta, Spika Mstaafu

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae.

Naomba sasa *Sergeant at Arms* uwaruhusu ndugu wa marehemu waweze kuingia humu ndani. Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka tulitengua Kanuni ili turuhusu ndugu wa marehemu 12 wajiunge nasi humu ndani, ambapo sita watakaa upande huu na sita watakaa upande ule.

Sergeant naomba uharakishe!

(Hapa Ndugu wa Marehemu waliingia ukumbini)

SPIKA: Katibu!

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:

MAELEZO YA SPIKA

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kama mtakavyokumbuka maelezo yangu ya leo asubuhi, niwakaribishe tena kwa Kikao Maalum cha kuaga mwili wa Marehemu Spika Mstaafu, Mheshimiwa Samuel Sitta. Hiki ni Kikao Maalum, kama nilivyosema, cha kuaga rasmi mwili wa Marehemu John Samuel Sitta, Spika Mstaafu wa Bunge la Tisa, kilichotokea usiku wa kuamkia tarehe 7 Novemba, 2016 huko Munich, Ujerumani.

Kikao hiki Maalum cha kipekee katika historia yetu kinafanyika kwa heshima yake, kama Spika Mstaafu, ambaye anapaswa kuzikwa kwa mazishi ya Kiserikali kwa mujibu wa Sheria ya Mazishi ya Viongozi ya Mwaka 2006. Shughuli zote za Kikao hiki Maalum zinaongozwa na orodha maalum ya shughuli za leo ambayo imetolewa na naamini Waheshimiwa Wabunge mnazo nakala zake. Katibu!

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:

MWILI WA MAREHEMU KUINGIA UKUMBINI

SPIKA: Sasa naomba *Sergeant at Arms* tuanze kwa kuingiza meza na baadaye nitawaomba Waheshimiwa Wabunge tusimame, wakati mwili wa marehemu ukiingizwa humu ukumbini.

(Hapa Meza iliingizwa ukumbini)

SPIKA: Sasa *Sergeant at Arms* tuletee mwili wa marehemu na naomba Waheshimiwa Wabunge wote tusimame pale tulipo.

(Hapa mwili wa Marehemu uliingizwa ndani ya Ukumbi wa Bunge)

Waheshimiwa Wabunge, naomba tuendelee kusimama. Katibu!

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:

WIMBO WA TAIFA

SPIKA: Naomba Wimbo wa Taifa upigwe.

(Hapa Wimbo wa Taifa Uliimbwa)

SPIKA: Tuendelee kusimama Waheshimiwa Wabunge. Sasa ni wakati wa Dua. Sasa namwita Mheshimiwa Dokta Yussuf Ali Suleiman, atafuatiwa na Mheshimiwa Shally Raymond. Mheshimiwa Dkt. Yussuf!

D U A

MHE. SULEIMAN ALLY YUSSUF: Habari za jioni ndugu zangu.

Alhamdulillah Rabbil Allah Amin, Wasswalatu Wassalaam alaa rasuli-llahi Muhammad Swalla-llahu Alayhi Wasallam, Wabaa'd.

Ndugu zangu, tumekutana hapa jioni hii kuomboleza kifo cha kiongozi wetu, lakini ninachotaka kuwakumbusha ni kwamba kifo si kitu cha ajabu kwa sababu kifo ni mlango ambao kila mmoja miongoni mwetu lazima aingie. Mwenyezi Mungu Subhanahu-Wata'ala anatuambia katika Qurani, *Kullu nafsin dhaikatul-maut* (kila nafsi itaonja mauti), hakuna miongoni mwetu ambaye atasalimika, si kwa sababu ya cheo au utajiri au kwa chochote kile, lazima mlango huo tuingie. Mwenyezi Mungu anatuambia *aina maatakunu yudrikum-lmaut walakuntum fi buruji mushayyadah* (popote mtakapokuwepo basi mauti ni lazima yatawafika, hata kama mngalikuwa katika ngome ambazo zimeimarishwa ulinzi kiasi gani ni lazima mauti yawafike). Lakini ajabu tu ni namna ya kuishi katika dunia hii, unatakiwa uishije.

Mtume wetu Muhammad Swala-llahu aleyhi wasallam katuambia *kun-fi dduniya ka-annaka gharib au-adiru ssadir* (ishi au kuwa katika dunia hii kama vile wewe ni mgeni au mpita njia). Kawaida ya mpita njia huwa hafanyi jeuri na kibri. Ndugu zangu kibri, jeuri ni vitu ambavyo havifai kabisa kabisa kwa sababu

maisha ya dunia hii, kama anavyosema Mwenyezi Mungu, *wamal-hayatu dduniya ila matau-lghurur.* Haya maisha ya dunia si chochote isipokuwa ni starehe za kudanganya, tunajidanganya sisi wenyewe. Kwa hivyo ndugu zangu wafiwa tustahimili sana na tujue kwamba hii ni njia ambayo na sisi tutapita.

Turudi kwenye Dua tumuombee Marehemu. Ewe Mwenyezi Mungu mwingi rehma, Mwenyezi Mungu mwingi wa kusamehe, Mwenyezi Mungu mwenye elimu, mjuzi wa kila kitu, unamjua sana mja wako huyu kuliko tulivyokuwa tunamjua sisi. Lakini sisi katika dhana yetu ni kwamba mja wako huyu alikuwa ni mwema sana. Katenda mengi mema ambayo tumeyaona kwa ajili ya nchi yake na kwa ajili ya watu wake. Mwenyezi Mungu tunakuomba kwa uwezo wako umlipe kwa yale mema yake aliyoyatenda, tunakuomba ewe Mwenyezi Mungu umuweke mahala anapostahiki kulingana na amali zake. *Wasalla-llahu alaa Muhammad Waala Allyihi waswahabihi wasallam, Alhamdulillah.*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Yussuf Ally Suleiman, sasa naomba Mheshimiwa Shally Raymond ajiandae, aje hapa mbele, na Mheshimiwa Harrison Mwakyembe ajiandae.

MHE. SHALLY J. RAYMOND: Tuombe! Ni katika jina la Baba, Mwana na Roho Mtakatifu Amina! Ee Mungu Mtakatifu! Mtakatifu! Mtakatifu! Uliye juu ya yote siku zako hazina mwisho na rehema zako hazina idadi. Tunakuomba utukumbushe daima kwamba maisha ya hapa duniani ni mafupi, na ya kwamba hatujui siku wala saa tutakapokufa. Tunakuomba Roho wako Mtakatifu atuongoze katika utakatifu na haki siku zote za maisha yetu, tufike salama katika Ufalme wako.

Baba Mwema, wakati huu umependa kumwita kwako huyu ndugu yetu Samuel John Sitta kutoka uzima huu baada ya kuwa nasi kwa nyakati tofauti. Kwa kuwa aliishi akimwamini Kristu aliyefufuka wa kwanza kutoka wafu, tunamuomba Mungu ampokee katika imani yake na mwili wake aufufue siku ya mwisho kwani mwili wake ulikuwa hekalu ya Mungu toka siku aliyobatizwa kwa maji. Tunakuomba Ee Bwana umsamehe makosa yake yote.

Nanyi ndugu zangu mliokusanyika hapa mumsamehe pale alipowakosea, nikianzia na familia yake, mama yake mzazi, mke, watoto, jamaa, ndugu na marafiki; Waheshimiwa Wabunge, Watumishi wa Bunge, Wana-Urambo na wote aliokutana nanyi katika maeneo ya kazi wakati wa utumishi wake wa kulijenga Taifa hili la Tanzania; kwani ni katika kusamehe tu nasi tutasamehewa.

Twakuomba Ee Bwana umpokee huyu ndugu yetu katika uzima wa milele, apate furaha isiyo na mwisho na kukaa miongoni mwa Watakatifu wote, daima na milele.

Tunajiombea na sisi wenyewe tulio bado na pumzi ili tupate kutenda mema kuwapendeza wenzetu na kukupendeza wewe Mwenyezi Mungu muumba wetu sote mpaka utakapotuita kwako.

Tunaomba hayo kwa Njia ya Kristu Bwana wetu Amina.

Raha ya Milele umpe Ee Bwana, na Mwanga wa Milele umuangazie! Apumzike kwa amani.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Shally Raymond. Kama mlivyoona dua ya kwanza ilikuwa kwa madhehebu ya Kiislam na dua ya pili imekwenda kwa taratibu za Kanisa la *Roman Catholic*. Sasa ninamkaribisha Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe akiwakilisha *CCT.*

MHE. DKT. HARRISON G. MWAKYEMBE: Tuombe, Baba Mwenyezi Mungu muumba mbingu na dunia umetufundisha kushukuru kwa kila jambo. Na mimi hapa Baba nasimama mbele ya umati huu, kukushukuru ee Bwana, kwa ajili ya Samuel Sitta. Ni wewe mwenyewe Baba uliyemleta duniani Samuel Sitta, ni wewe mwenyewe Baba uliyempa Samuel Sitta kipaji kikubwa cha uongozi, uliyempa Samuel Sitta kipaji kikubwa cha kuongoza watu wako, kuwatumikia watu wako kwa uadilifu mkubwa , unyenyekevu mkubwa kwa ujasiri na uthubuti wa hali ya juu.

Baba Mwenyenzi Mungu, ni wewe uliyempa moyo Samuel Sitta wa kuwatetea wanyonge, na kuwapigania na kupambana na wale wote waporaji wa rasilimali za Taifa. Na baba Mwenyenzi Mungu kila alipopita mtoto wako Samuel Sitta, aliacha alama za uongozi uliotukuka.

Baba na Bunge hili kuta zote, hata sakafu, viti tunavokalia, vinashuhudia kazi kubwa aliyofanya Samuel Sitta katika Bunge hili. Baba Mwenyenzi Mungu, niseme nini kuhusu Samuel Sitta kwa yote aliyoyafanya?

The Name of Samuel Sitta speaks for itself in this August Assembly. Sisi tungeomba Mungu Samuel Sitta aendelee kuwepo kwenye uhai, lakini nisamehe Baba kwa sababu umetufundisha kwamba tushukuru kwa kila jambo. Wewe umempenda zaidi na Baba mimi nani kuuliza hilo kwani umechuma ua la waridi katika bustani yako, mapenzi yako yatimizwe.

Baba Mwenyenzi Mungu, mimi ni mmoja wa Watanzania wengi sana waliopendelewa na kusaidiwa kwa kila hali na Marehemu Samuel Sitta, uliyempa mkono wa kutoa, uliyempa moyo wa huruma, moyo wa mapenzi ya hali ya juu. Alinifundisha nilipoingia kwenye siasa, akasema mdogo wangu siasa siyo sayansi, *in science, the higher you go, the colder becomes but the politics*

the higher you go the hotter it becomes. Kwa hiyo, mdogo wangu jioteshee ngozi nene ili ukienda juu usiathirike na joto, ukishuka chini usiathirike na baridi.

Baba Mwenyenzi Mungu nakushukuru kwa yote kuhusu maisha ya Samuel Sitta, nikuombe kitu kimoja tu baba, mikuombe kitu kimoja tu! Na naomba unisikie Baba. Baba iweke Roho ya Samuel Sitta, pema peponi Amen.

(Hapa Wabunge na Wageni waliokuwepo ndani ya Jengo la Bunge walilia)

SPIKA: Naomba Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu!

DKT. THOMAS D. KASHILILAH-KATIBU WA BUNGE: Wasifu wa Marehemu.

SIPKA: Sasa naomba tupate kusikia Wasifu wa Marehemu na hivyo, naomba nimwite Mheshimiwa Naibu Spika, Dkt Tulia Ackson. Mheshimiwa Naibu Spika tafadhali.

WASIFU WA MAREHEMU

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Viongozi wote, wafiwa wote, Mheshimiwa Margaret Sitta, Waheshimiwa Wabunge na wageni wote. Nitasoma wasifu wa Marehemu Samuel Sitta, Spika Mstaafu wa Bunge la Tisa la Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kwa niaba ya Mheshimiwa Spika.

Marehemu alizaliwa tarehe18 Disemba,1942, huko Urambo Tabora. Kuhusu elimu yake; marehemu Samuel Sitta alianza shule ya msingi mwaka 1950 katika shule ya msingi Urambo. Mnamo mwaka 1953 Marehemu Mzee Sitta aliendelea na elimu ya msingi katika shule ya Sikonge, *middle school* ambako alisoma mwaka 1954-1957.

Marehemu Sitta alijiunga na Shule ya Sekondari ya Wavulana ya Tabora, *(Tabora Boys Secondary School)* mwaka 1958 ambako alisoma kidato cha kwanza hadi kidato sita, ambapo alihitimu mwaka 1963. Mnamo mwaka 1964, Marehemu Mzee Sitta, alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambako alihitimu shahada ya Sheria mnamo mwaka mwaka 1971. Marehemu Mzee Sitta, alijiendeleza kielimu, ambapo mwaka 1976, alihitimu diploma katika masuala ya utawala nchini Uswiss. Mwaka 2014 alipata cheti ya mafunzo ya uongozi kutoka Chuo cha Harvard nchini Marekani.

Maisha ya Ndoa; Marehemu Mzee Sitta, alifunga ndoa na Bi Margaret Simwanza Sitta, ambaye kwa sasa ni Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Urambo Mashariki, ndoa hiyo ilifungwa mwaka 1968 na wamejaliwa watoto watano.

Historia katika Utumishi wa Umma; Marehemu Mzee Sitta, alianza kazi mnamo mwaka 1967, akiwa ni Meneja wa Kampuni ya *Caltex Oil*, ambapo

mwaka 1969 aliajiriwa na Shirika la Maendeleo ya Taifa *(National Development Cooperation)* akiwa ni Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi na Mkurugenzi wa Utawala hadi mwaka 1975, alipochaguliwa kuwa Mbunge na kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Mawasiliano.

Marehemu Mzee Sitta, alishikilia nafasi mbalimbali za Uwaziri kati ya mwaka 1975 mpaka mwaka 1995 ikiwemo Waziri mwenye dhamana ya Ustawishaji Makao Makuu, Waziri wa Sheria na Waziri wa Ujenzi, ikiwemo pia kuteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro na Iringa katika kipindi hicho.

Ni katika uongozi wake kama Waziri Ujenzi ndiyo daraja maarufu kama *Selander Bridge* lilijengwa, mwaka 1980 na pia uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere ulijengwa mwaka 1981. Mnamo mwaka 1996, Marehemu Mzee Sitta, alikuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji *(Tanzania Investment Center)* ambako alihudumu hadi mwaka 2005.

Katika uongozi wake kwenye Kituo cha Uwekezaji Tanzania, kituo hicho kilichaguliwa kuwa kituo bora cha uwekezaji Barani Afrika. Marehemu pia alikuwa ni Wakili wa Mahakama Kuu, akimiliki Kampuni ya Uwakili, iitwayo *Esco Law Chambers.*

Utumishi wake katika siasa; Marehemu Mzee Sitta, alikuwa mwanachama wa TANU, na baadaye Chama cha Mapinduzi mwaka 1977, ambako pia alishikilia nafasi mbalimbali za uongozi hadi mauti yalipomkuta.

Kuanzia mwaka 1987-1988, Marehemu Mzee Sitta, alikuwa Katibu Mtendaji wa CCM Mkoa wa Iringa na mwaka 1990-1993 alikuwa Katibu Mtendaji wa CCM, Mkoani Kilimanjaro. Marehemu alikuwa Mjumbe wa Kamati Kuu kati ya mwaka 2005 hadi 2010 na mpaka anafariki, Marehemu Mzee Sitta, alikuwa ni Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya Chama cha Mapinduzi.

Marehemu Mzee Sitta, alikuwa Mbunge wa Urambo na baadaye Urambo Mashariki Jimbo hilo lilipogawanywa kwa vipindi mbalimbali, kati ya mwaka 1975 mpaka 2015. Marehemu Mzee Sitta alichaguliwa kuwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2005 nafasi aliyoishikilia hadi mwaka 2010 akijulikana na maarufu sana kwa sifa yake ya Uspika wa kasi na viwango *(speed and standards)*

Marehemu aliteuliwa kuwa Waziri wa Afrika Mashariki, tarehe 24 Novemba, 2010, nafasi aliyoishikilia hadi tarehe 25 Januari, 2015, alipoteuliwa kuwa Waziri wa Uchukuzi, nafasi aliyohudumu hadi Oktoba, 2015 ilipoanza Serikali ya Awamu ya Tano.

Marehemu Mzee Sitta alichaguliwa kuwa Mwenyekiti, wa Bunge la Katiba wakati lilipoundwa kwa minajili ya kupata Katiba Mpya ambayo kwa sasa tuliyonayo ni Katiba Inayopendekezwa mnamo mwaka 2014.

Marehemu Mzee Sitta, amewahi pia kushika nafasi za uongozi katika Vyama vya Kibunge duniani, ikiwemo kuchaguliwa kuwa Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Chama cha Wabunge wa Jumuiya ya Madola, Makamu wa Rais na baadaye Rais wa Dunia wa chama hicho mwaka 2008 na 2009.

Kuhusu ugonjwa; Marehemu Mzee Sitta, alikuwa akisumbuliwa na tatizo la tezi dume, ambapo alipata matibabu hapa nchini, baadaye aliendelea kupata matibabu nchini India na Uingereza na hatimaye nchini Ujerumani ambako alienda mara kadhaa.

Marehemu Mzee Sitta, alikwenda nchini Ujerumani kwa mara ya mwisho tarehe 3 Novemba, 2016 na kulazwa katika Hospitali ya *Clinic of Nuclear Medicine, Technical University of Munich,* Mjini Munich ambapo usiku wa kuamkia tarehe 7 Novemba, 2016, marehemu Mzee Sitta aliaga dunia akiwa na mkewe bibi Margaret Simwanza Sitta, Mbunge.

Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

SPIKA: Ahsante Sana Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Naibu Spika, kwa wasifu huo wa ndugu yetu, mzee wetu, kiongozi wetu. Katibu!

DKT. THOMAS D. KASHILILAH- KATIBU WA BUNGE: Salamu za Rambirambi.

SPIKA: Sasa tunaingia katika kipindi cha salamu za rambirambi, nitawaomba sana wale mtakaopata fursa msizidi dakika tano. Tutaanza na Mheshimiwa Zitto Ruyagwa Kabwe, kwa niaba ya Chama cha *ACT* Wazalendo.

MHE. KABWE Z. R. ZITTO: Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, Mama Margaret Sitta, watoto wote wa Mzee Samuel John Sitta, ndugu, jamaa na marafiki,

Ndugu zangu Watanzania, leo kikao maalum cha Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Mkutano wake wa Tano, kinamuaga mtoto wa Mzee John Sitta na Hajat Zuwena Said Fundikira. Nami nimepewa nafasi niseme maneno machache kuhusu mzee wetu tunayemuaga leo.

Samuel John Sitta, anayo mengi, lakini Tanzania itamkumbuka kama mtu aliyejaribu kuboresha kila jukumu alilokabidhiwa. Shujaa wa wote wanaoamini katika uwajibikaji wa kitaasisi, mwanasiasa aliyepanda na kushuka na kupanda

na kubakia kileleni, taswira ya Mkoa wa Tabora sio tu mdhamini wa *club* ya Simba, bali pia mwana Simba aliyeipeleka *club* Brazil na kuwezesha kuifunga Yanga mabao mengi zaidi ambayo hayajapata kulipwa na wapinzani wetu hata kwa kuungaunga, mwana mageuzi wa Bunge na Spika wa mioyo ya Watanzania. *(Makofi)*

Hata katika kifo chake, Samuel John Sitta, ameweka rekodi nyingine; kwa Bunge kufanya kikao maalum kuenzi mmoja wa wajumbe wake mahiri kati ya mwaka 1975 na mwaka 2015 isipokuwa tu kwa kipindi cha 1995 mpaka mwaka 2005. Rekodi hii itaendelea kwa wengine wote watakaofuata baada yake. *(Makofi)*

Ni mtu wa namna gani wewe Samuel Sitta; Spika wa kasi na viwango, unayeweka rekodi hata ukiwa umelala ndani ya jeneza lako lililopambwa na bendera ya Taifa letu, ukielekea nyumbani kwako Urambo kwenye nyumba yako ya milele. Ulikuwa hushindwi ukiwa hai, umeonyesha umahiri wako hata ukiwa kwenye umauti, kweli wewe ni Spika wa watu, *the people Speaker*. *(Makofi)*

Tuliokupenda tunajua, ulikuwa baba mlezi, ulikuwa mume mwema, ulikuwa babu, ulikuwa kiongozi, nadhani hata kwa uliokwaruzana nao hapa na pale wanajua hilo. Leo sote tuna majonzi makubwa, umeliunganisha Taifa katika kukukumbuka ewe Spika wa watu. Ulikuwa na vyeo vingi, Mbunge, Naibu Waziri, Waziri, Mkuu wa Mkoa, Waziri tena, Mkurugenzi Mtendaji, Spika, Waziri tena na Mwenyekiti wa Bunge la Katiba lakini wala, tunakuita Spika Sitta tu! Kwa nini? Kwa sababu ya *legacy* yako ni Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Sio kwamba wewe umeanzisha Bunge la hasha, lakini ulipopokea Uspika wa Bunge letu, kama ilivyo jadi yako, ulililboresha, uliwezesha kutunga kanuni mpya, uliimarisha mhimili huu na kuuweka katika nafasi yake ya Kikatiba. *(Makofi)*

Nakumbuka siku moja ulimwomba Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aongee na baadhi yetu ilikuwa mwaka 2006. Mimi nilikuwa na miaka 29 tu, tukakutana na Rais ukumbi wa Msekwa, baada ya kikao kilichofanikiwa kumshawishi Rais kuhusu mabadiliko uliyoyataka, uliniambia, babu, mimi sasa alasiri, ninyi ndio saa nne asubuhi, naweka misingi tu na kuliweka Bunge katika nafasi yake ya kikatiba. *(Makofi)*

Kilichofuata ni mabadiliko makubwa ya Kanuni za Bunge, kuandikwa upya kwa sheria ya Bunge, *(National Assembly Administration Act)* na kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo wa Majimbo *(Constituency Development Catalyst Fund). (Makofi)*

Samuel Sitta bado tunasikia mwangwi wa sauti yako nene kutoka kwenye kiti cha Spika, ukiwataka Mawaziri wajibu maswali kwa ufasaha. Hukuisahau Tabora yako, damu ya kichifu wa Unyanyembe ya Fundikira kutoka kwa mama yako Zuwena ilikusambaa kwenye mishipa yako, ukiona kuna swali linalohusu Mkoa wako wa Tabora, hukusita kuwaambia Mawaziri wajibu vizuri hasa kuhusu barabara. Au ukiamsha jeshi lako la akina Lucas Lumambo Selelii, wakisema Mheshimiwa Spika, wewe leo ukipata dharura Urambo unafikaje? Yote hiyo ni kutilia nguvu umuhimu wa maendeleo ya mkoa wako. *(Makofi)*

Wewe ni kielelezo cha Demokrasia ya Vyama vingi Bungeni, ulitoa nafasi kwa Wabunge wote wa Kambi zote ndani ya Bunge, hatusemi hukubagua la hasha! U-CCM wako ulikuwa pale pale, lakini walio wengi walishinda na walio wachache walisikika, ndio demokrasia. *(Makofi)*

Mzee Sitta, ulikuwa muungwana, nakumbuka siku ile unamwomba radhi Mzee John Mamose Cheyo, katika Kamati ya Uongozi baada ya kuwa ulimtoa kwa makosa Bungeni, ukaseme eti msongo wa mawazo ulikujaa, watu walikuwa wanapita pita jimboni kwako, lakini uliwashinda. Unyenyekevu wako wa kuomba radhi unapokosea ni somo kubwa sana kwa viongozi wengine. *(Makofi)*

Wabunge wenzangu tunataka kumuenzi Spika wa watu, Samuel John Sitta? Basi hakuna kumuenzi bora zaidi kama kuimarisha uhuru na heshima ya Bunge letu.

Tuendeleze jahazi, Samuel Sitta anakwenda kwenye nyumba yake ya milele akiongozwa na imani yake kubwa kwa Mungu na uzalendo wako usio na mawaa kwa nchi yeke Tanzania, angalau bado ataendelea kuwa nasi kwa kutuachia mafundisho makubwa kutokana na maisha yake. Mambo mema aliyoyafanya kwa nchi yetu, ndoto aliyoiishi ya Tanzania imara na yenye heshima na malezi kwa viongozi wengi vijana aliowafunda na kuwalea kiuongozi. *(Makofi)*

Ni dhahiri umeishi maisha yako babu, kama isemavyo katika biblia katika Timotheo; nimepigana vita vilivyo vizuri mwendo nimeumaliza, imani nimeilinda. Tangulia Spika wa watu, *the people's speaker*, tangulia Spika wa Bunge la wananchi, tangulia Samuel John Sitta. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Zitto Ruyagwa Kabwe. Naomba nimwite Mheshimiwa Riziki Shahari Mngwali, kwa niaba ya Chama cha *CUF*. Mheshimiwa Riziki!

MHE. RIZIKI S. MNGWALI: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, mpendwa wetu,

Mama Margaret na Waheshimiwa Wabunge; nimesimama mbele yenu hapa kwa niaba ya Wabunge wa Chama cha Wananchi *(CUF)* kutoa salaam zetu za pole na kushiriki nanyi katika msiba huu mzito ambao umemgusa kila mmoja wetu.

Mheshimiwa Spika, tunaomba pia mama yetu Hajjat Zuwena uliko, Mwenyezi Mungu akufariji na akupe nguvu ya kuhimili msiba huu mzito, wewe pamoja na mwanao mpenzi mama Margaret, mhimili kipindi hiki kizito. Uliwaambia umma kupitia vyombo vya habari; Hajjat Zuwena ulikuwa na watoto wawili tu, kipenzi chako kimoja Samuel Sitta amekutangulia. Hukutarajia hivyo, lakini ulikubali kwa sababu ni mapenzi ya Mwenyezi Mungu. Tunamwombea Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu wetu huyu pale hasa anapostahiki.

Mheshimiwa Spika, binafsi sikuwahi kumfahamu marehemu kwa ukaribu, lakini Waheshimiwa Wabunge aliokuwa nao wa Chama cha Wananchi *(CUF)* mwaka 2005 na kipindi chote ambacho aliwaongoza, watumishi wa Bunge hili Tukufu waliowahi kuwa hapa wakati Mheshimiwa marehemu wetu Samuel Sitta akiwa Spika hasa watumishi wenyewe wanaojiita wanyonge, wanamtaja kwa moyo wa kumkumbuka kwa wema aliowatendea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wabunge waliokuwepo enzi za marehemu Sitta wanasema alikuwa ni Spika ambaye mlango wake ulikuwa wazi kwa shida zote za Waheshimiwa Wabunge; shida ndogo kwa kubwa. Hakuna hata shida moja aliyosema ni ndogo haistahili kufika kwake na hakuna hata shida moja kubwa aliyosema iko juu ya uwezo wake. Waheshimiwa Wabunge hao wameniambia mimi ambaye sikuwahi kuwa na marehemu, kwamba marehemu Samuel Sitta alikuwa Spika, alikuwa kiongozi kwa ajili ya Wabunge hao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nasimama hapa kwa heshima kubwa, kama nilivyosema mwanzo kwa niaba ya Wabunge wa Chama cha Wananchi *(CUF)* kumwombea marehemu wetu huyu Mwenyezi Mungu amlipe kwa haya mema aliyowatendea waja wake, kwani ni ahadi yake Mwenyezi Mungu kwamba kila aliyewasaidia wanyonge, viumbe vya *Allah* basi naye atamsaidia katika njia zake za duniani na huko akhera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunamuomba Mwenyezi Mungu amweke marehemu mzee wetu Samuel Sitta pale anapostahiki. Hakika sisi wote ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea. Mzee wetu Sitta ametangulia katika safari hiyo. Ahsanteni! *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Bi. Riziki Shahari. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Tundu Lissu kwa niaba ya CHADEMA. Mheshimiwa Tundu Lissu, Mnadhimu Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni!

MHE. TUNDU A. LISSU: Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kumpa pole sana Mheshimiwa Mama Sitta pamoja na watoto wa Mzee Sitta na ndugu zake na wananchi wake wa Jimbo la Urambo pamoja na Waheshimiwa Wabunge ambao aliwatumikia kwa muda mrefu sana.

Mheshimiwa Spika, tumekutana hapa leo ili kukumbuka mmoja wa miamba ya Tanzania, kwa sababu Samuel John Sitta alikuwa mmoja wa miamba ya Tanzania. Tumekutana hapa leo kumkumbuka mmoja wa miamba ya Bunge hili, kwa sababu Samuel John Sitta alikuwa mmoja wa miamba ya Bunge hili. Pengine ni haki na pengine ni sawasawa kwamba, tunafanya kumbukumbu hii ndani ya ukumbi huu ambao Samuel John Sitta aliutawala kwa umahiri mkubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pengine ni sawasawa na ni vyema kabisa, katika historia ya Bunge la Tanganyika *Territory* na katika historia ya Bunge la Tanzania, Samuel John Sitta atakuwa ni Spika wa kwanza wa Bunge kufanyiwa heshima na kumbukumbu ambayo tunamfanyia leo hii humu ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Samuel John Sitta alikuwa mtumishi wa umma wa miaka mingi sana; sifa zake zimezungumzwa sana; lakini historia ya nchi hii, historia ya watoto wa watoto wetu, miaka 200, 300 baada ya kuwa tumeondoka hapa, itamkumbuka Samuel John Sitta kwa miaka yake mitano akiwa Spika wa Bunge hili kati ya mwaka 2005 hadi mwaka 2010. *(Makofi)*

Katika historia ya Bunge hili, kwa muda mrefu, Bunge kwanza la Chama kimoja na baadaye Bunge hili la Vyama vingi liliishi katika kivuli cha Serikali, liliishi *under the shadow of the Executive*. Samuel John Sitta aliliondoa Bunge la Tanzania kutoka katika kivuli hicho. Samuel John Sitta alilifanya Bunge kuwa Bunge la Tanzania linalofahamika leo. Kwa sababu hiyo, tunapomkumbuka Samuel John Sitta, kama nilivyosema, utumishi wake mkubwa na wa muda mrefu, kile kitu Waingereza wanaita *the shell on the cake;* ni miaka mitano ya Uspika wake katika Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Samuel John Sitta alitaka Bunge lenye meno; Samuel John Sitta alitaka Bunge linaloisimamia na kuidhibiti Serikali; Samuel John Sitta alitaka Bunge kama Mhimili wa Dola na siyo msindikizaji wa mihimili mingine ya dola. Hii ndiyo zawadi kubwa ya utumishi wake mrefu kwa Tanzania, ni rekodi yake ya miaka mitano kama Spika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Samuel John Sitta hakuwa kibaraka wa mtu yeyote; na tunasema ukisoma wasifu hausemi mengi, lakini tangu akiwa kijana, Samuel Sitta alionesha kuwa ni mtu mwenye msimamo huru. Huo msimamo huru, ndiyo uliomfanya aliweke Bunge letu katika ramani ya kisiasa ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa tunapomkumbua Samuel John Sitta kwa utumishi wake uliotukuka, ni vyema na ni sawasawa tukalia kama ambavyo tunalia humu ndani; ni vyema tukahuzunika kama ambavyo tunahuzunika humu ndani leo; ni vyema tukajisikia vibaya kama ambavyo kila mmoja wetu anajisikia vibaya leo hii; lakini hii haitoshi. Kilio, majonzi na huzuni havitoshi.

Mheshimiwa Spika, kwa maoni yetu, namna bora ya kumkumbuka Samuel John Sitta ni kujiuliza, hili ni Bunge ambalo alilitaka? Hili ni Bunge ambalo alitaka liwe? Hili ni Bunge ambalo angetaka kuliongoza? Tukijiuliza maswali hayo, tukayatafutia majibu yake, tutakuwa tumemkumbuka Samuel John Sitta kwa namna inayomstahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kurudia tena kumpa pole sana mama na kuwapa pole sana watoto wa Mzee Sitta na kuwapa pole Watanzania kwa kuondokewa na jabali hili la siasa za nchi hii. Nashukuru sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Tundu Mughwai Lissu. Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, kwa niaba ya Chama cha Mapinduzi.

MHE. JASSON S. RWEIKIZA: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Chama cha Mapinduzi Bungeni, napenda kukupa salamu za pole kwako wewe binafsi, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge wote kwa msiba huu mkubwa wa kuondokewa na mpendwa wetu, Mheshimiwa Samuel Sitta.

Tulipokea taarifa za kifo cha Mheshimiwa Sitta kwa mshituko na majonzi makubwa sana. Napenda kutoa pole kwa wananchi wa Jimbo la Urambo ambalo Mheshimiwa Sitta alikuwa Mbunge kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, natoa pole sana kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na Waheshimiwa Marais wastaafu wote na viongozi wote aliofanya nao kazi pamoja Marehemu Mheshimiwa Sitta. Natoa pole kwa Watanzania wote kwa kufiwa na mpendwa wetu Mheshimiwa Sitta.

Mheshimiwa Sitta katika uongozi wake alikuwa mwadilifu na mzalendo wa kweli kweli. Kipekee natoa salamu nyingi za pole kwa familia ya marehemu ikiongozwa na Mheshimiwa Margaret Sitta, Mbunge mwenzetu kwa msiba mkubwa wa kuondokewa na mume wake mpendwa. Tunawaombea Mwenyezi Mungu awape neema ya uvumilivu wewe Mama Sitta, familia, ndugu na marafiki wote kwenye kipindi hiki kigumu na chenye majonzi makubwa.

Chama cha Mapinduzi Bungeni tumepoteza kiongozi mwadilifu. Mheshimiwa Sitta alikuwa mchapakazi hodari aliyejituma na asiyechoka; hakuwa mtu wa kupenda kujinufaisha binafsi, bali kulinufaisha Taifa. Hakuwa mpenda majungu, alikuwa na upendo wa kweli na alipigania wanyonge kama ilivyo misingi ya Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi tuliomkuta Bungeni tulimtumia kama kisima cha uzoefu na utajiri wa hekima. Tulijifunza kwake mambo mengi sana mazuri kama kufanya kazi kwa kasi kubwa na viwango vya juu *(speed and standards)*. Ni kwa sababu hii Mheshimiwa Sitta aliweza kufikia ngazi ya juu ya utumishi katika Taifa hili ikiwa ni pamoja na kuwa Spika wa Bunge la Tanzania, Mwenyekiti wa Bunge Maalum la Katiba, Waziri, Mkuu wa Mkoa na nyadhifa nyingine nyingi. Nawaomba Watanzania wenzangu tumuenzi Mheshimiwa Sitta kwa kufanya na kuendeleza mambo mazuri yote aliyoyafanya kwa Taifa hili. *(Makofi)*

Mwenyezi Mungu alitoa, Mwenyezi Mungu ametwaa, jina lake lihimidiwe. Tumwombee ndugu yetu Mzee Sitta Mwenyezi Mungu amweke mahali pema peponi. Amina.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, ambaye pia ni Katibu wa Wabunge wa CCM ndani ya Bunge. Naomba sasa kwa fursa hii nimwite Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe kwa salamu zake.

MHE. FREEMAN A. MBOWE: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waheshimiwa Wabunge wote, mpendwa sana Mama yetu, Dada yetu Mheshimiwa Margaret Sitta, watoto wote wa marehemu, ndugu, marafiki, jamaa na waombolezaji wenzangu; nawashukuru sana wazungumzaji wote walionitangulia kwa sababu wameyaeleza yale yote yaliyomstahili Mzee wetu Mheshimiwa Sitta.

Mheshimiwa Spika, nitajaribu kujazia kidogo tu, kwa namna ambavyo sisi wengine tulimwona na kumtafakari Mzee Sitta, sisi kama Kambi ya Upinzani ndani na nje ya Bunge tulimwona Mzee Sitta kama kiongozi asiyekuwa mbaguzi wa kiitikadi; na tulimwona Mzee Sitta kama kiongozi ambaye ni *reformist*. Aliamini katika kubadilisha kwenda kwenye ubora, katika nafasi yoyote ya Utumishi wa Umma ambayo aliweza kuihudumia. Mzee Sitta alikuwa mtu aliyejaza matumaini watu wote aliowaongoza wakati wote. Alikuwa *catalyst of hope*. *(Makofi)*

Mzee Sitta alikuwa ni mtu wa kuunganisha makundi yote; alikuwa ni *symbol of unit*. Mara nyingine sisi Wapinzani tulipata wakati mgumu sana wa kumtambua Mheshimiwa Sitta bado ni kada wa Chama cha Mapinduzi; kwa sababu alikuwa na uwezo wa kutujaza matumaini, kutupa fursa ya kutusikiliza,

lakini mwishoni tunakuja kugundua kumbe bado Mzee Sitta ni wa Chama cha Mapinduzi. *(Makofi/Kicheko)*

Mzee huyu aliamini katika kupigania haki za kila aliyemwongoza. Wote ni mashahidi, Mzee Sitta hakusita wakati wowote kutaka Bunge hili lisimame kama mhimili ambao unaidhibiti na kuisimamia Serikali, lakini wakati huo huo hakusita kuitetea Serikali alipoona Serikali inastahili kutetewa. Hakuwa mwoga kupigania alichokiamini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Mzee Sitta anatutangulia mbele ya haki, amepigana maisha yake, amepigana vita yake na safari yake ameimaliza.

Mheshimiwa Spika, tunajifunza nini kwenye maisha ya Mzee Sitta? Tunaweza tukalia sana na tukaomboleza mno na ni haki yetu tufanye hivyo kwa sababu mzee huyu alikuwa na sifa zote na alistahili kufanyiwa anachofanyiwa leo.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, leo asubuhi tumemuaga tena kiongozi mwenzetu ambaye amekwenda kuzikwa Zanzibar, Mheshimiwa Hafidh Ali. Nilisema asubuhi na sasa naomba nirudie tena, leo ni siku ambayo Mungu ametupa Wabunge na viongozi wa umma nafasi ya kutafakari dhamana aliyotupa ya kuwaongoza wenzetu. Kila mmoja unapopata dhamana ya kuwaongoza wengine, hao unaowaongoza watakungumzaje siku wanakuaga? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spka, leo hatumpambi Mzee Sitta kwa sababu ni utaratibu wa misiba, tunazungumza kwa dhati ya roho zetu, tunazungumza kwa dhati ya mioyo yetu kwa sababu Mzee Sitta aliwaunganisha Wabunge wote japo ametuachia kazi moja kubwa ambayo tuliobaki tunastahili kuimalizia. Mzee Sitta ametuachia kazi ya Katiba, alikuwa Kiongozi wetu katika Bunge la Katiba, kazi ambayo wote tunajua hatukuikamilisha, lakini Taifa bado linahitaji tuwapatie Katiba ambayo itawaunganisha wananchi, itatuunganisha wote kuwa Taifa moja linalopendana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ndugu zangu viongozi wenzangu, tunapomwomboleza Mzee wetu Samuel Sitta tukumbuke kwamba vyeo vyetu ni dhamana na ni vitu vya kupita lakini maisha yetu wote tutaendelea kuwa wamoja na kama Watanzania tupendane, tusaidiane, tuheshimiane. Tusipendane tu wakati wa misiba, tupendane hata wakati wa maisha ya kawaida, tujenge Taifa lenye upendo. *(Makofi)*

Tunamshukuru sana Mungu kwa maisha ya Mzee Sitta. Mama yetu Margaret, wewe ni mama mpole, wewe ni mama mpatanishi. Wewe ni mama mnyenyekevu. Ni tunu alizokupa Mwenyezi Mungu. Mara nyingi umekuja ofisini

kwangu kuniambia kiongozi nisaidie tuwaunganishe akina mama katika Bunge. Hukuniona kama mwanao, uliniona kama kiongozi. *(Makofi)*

Tunakuombea sana Mama Margaret Mungu akujaze faraja, akupe uwezo wa kuvumilia sana. Natumaini Mama Margaret wewe ni mtu wa imani, wewe na familia yako Mungu atawavusha katika kipindi hiki kigumu katika maisha yenu. *(Makofi)*

Poleni sana Watanzania, poleni sana familia na ahsanteni sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbowe kwa hotuba yako.

Sasa naomba nimwite Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Kiongozi wa Wabunge walio wengi Bungeni, Mheshimiwa Waziri Mkuu! *(Makofi)*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Job Ndugai (Mb.), Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson (Mb.), Naibu Spika; Dkt. Thomas Kashililah, Katibu wa Bunge na watumishi wote wa Bunge; naomba nimtambue Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda ambaye tupo naye hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Waziri Mkuu Mstaafu; Mheshimiwa Freeman Mbowe (Mb.), Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni; Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge, Waheshimiwa Wabunge wote; Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam; Mheshimiwa Margret Sitta (Mb.), mjane wa marehemu na watoto wote pamoja na mama yake mzazi marehemu, Hajjat Zuwena Said Fundikira; Viongozi wa Dini mliopo hapa; Mabibi na Mabwana na Watanzania wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Serikali nianze kwa kuwapa pole mama yetu Mheshimiwa Margret Sitta (Mb.), muunganishi wa watu na mpenzi wa watu. Niwape pole watoto wa marehemu na mama wa marehemu Hajjat Zuwena Said Fundikira, ambaye bado yuko hai na ana nguvu ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wote ambao tuko kwenye Bunge hili, Serikali imepokea taarifa ya kifo cha Spika Mstaafu, Waziri na mtumishi aliyetukuka katika utumishi wake kwa mshtuko mkubwa sana. Historia ya Mzee Sitta ambayo ni kubwa na pana imezungumzwa na wale wote walionitangulia kuzungumza. Pia tunatambua utumishi wake uliotukuka katika nafasi mbalimbali ambazo zimetajwa kwenye wasifu wake. Utumishi huu

unaonyesha kwamba yeye ni mtu wa watu, kiongozi, mlezi na mtumishi mwadilifu katika kipindi chote cha uhai wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mengi yamezungumzwa na walionitangulia, sikusudii kuyarudia, tunaelewa hilo. Tutamkumbuka sana kwa mchango wake mkubwa kwa kuimarisha demokrasia, kusimamia ukweli na kutumia elimu na maarifa yake kwa manufaa ya wote ambao wameshuhudia utawala wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia historia ya maisha ya Mzee Sitta, hakika tunaweza kutumia siku na majuma kueleza, hatuna mengi ya kuongea kwa sasa, badala yake sisi tuliobaki tuzidi kumwomba Mwenyezi Mungu atusaidie, tuwe na maisha ambayo kwa imani zetu yatatuwezesha kufikia japo mema machache aliyoweza kutenda katika uhai wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii pia kutambua uwepo wa mzee wetu, Mzee Malecela, Waziri Mkuu Mstaafu, lakini pia tupo na Jaji Mkuu Mstaafu Mheshimiwa Agustino Ramadhani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hawa wote wanaungana pamoja nasi Wabunge na Watanzania wote leo hii kushuhudia kumpeleka nyumbani mzee wetu Mzee Sitta ili akapumzike kwenye nyumba yake ya milele. Niwapeni tena pole wote kwa ujumla, wanafamilia na Watanzania kwa msiba huu mkubwa ambao leo umegusa maisha ya kila mmoja wetu na wote waliokuja hapa wameeleza namna ambavyo umeweza kutugusa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina mengi ya kusema Bwana ametoa, Bwana ametwaa, Jina la Bwana libarikiwe. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Sasa ni wakati wa kutoa salamu zangu katika kuuaga mwili wa marehemu Mzee Samuel Sitta, Spika Mstaafu wa Bunge la Tisa.

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri Mkuu; Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni; Waheshimiwa Mawaziri; Waheshimiwa Viongozi wetu Wastaafu, Mzee Malecela, Mzee Pinda na Mzee Agustino Ramadhani; Mama Sitta na watoto wa marehemu; Mabibi na Mabwana wote mliojaa katika ukumbi huu.

Ni kwa masikitiko makubwa sana leo kwetu sote tuliopo hapa tunapomuaga mzee wetu na mpendwa wetu Mzee Samuel John Sitta, Spika wa Bunge la Tisa na Mbunge wa zamani wa Urambo na baadaye Urambo Mashariki kwa takribani miaka 20 alipotumikia kwa nafasi ya Ubunge. Siyo rahisi

kumweleze marehemu Mzee Samuel Sitta kwa muda huu mfupi tulionao kwani alikuwa na vipawa vingi na uwezo mkubwa wa uongozi.

Marehemu Mzee Sitta miongoni mwa sifa zake alikuwa kiongozi mwenye uthubutu. Aliposimamia jambo aliweza kujikwamua katika vihunzi na vigingi mbalimbali njiani. Nyote mnafahamu namna alivyofaulu katika kusimamia maendeleo ya Bunge la Tisa. *(Makofi)*

Aliweza kusimamia mabadiliko, maboresho na hivyo katika Bunge la Tisa tulikuwa na Bunge makini lenye demokrasia ya ndani na lenye uwezo wa kuishauri na kuisimamia Serikali kutimiza wajibu wake kwa wananchi kwa misingi ya haki na kwa ufanisi mkubwa. Aliyafanya haya akiwa na kaulimbiu yake iliyomfanya ajulikane kwa sifa ya Mzee wa Kasi na Viwango *(Speed and Standards)*. *(Makofi)*

Kwangu mimi huzuni hii ni mara dufu kwa vile Mzee Sitta alikuwa mlezi wangu na mwalimu wangu. Akiwa Spika mwaka 2005 - 2010, mimi nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Ardhi, Maliasili na Mazingira na pia Mwenyekiti wa Bunge nikimsaidia kazi hapa Mezani katika Kiti cha Uspika. *(Makofi)*

Nilijifunza mambo mengi kwa miongozo, maelekezo na ushauri alioutoa kwangu. Alikuwa ni nahodha mwenye kujali timu yake ya hapa Mezani, akitupa nafasi kubwa ya kufanya kazi zetu kama Wenyeviti wa Bunge kwa kutupa fursa za kukaa Mezani mara kwa mara na kwa uhuru mkubwa zaidi. *(Makofi)*

Katika Bunge la Tisa lenye mafanikio ambayo Watanzania hupigia mfano, Mzee Sitta kazi hii hakuifanya peke yake, alikuwa na Wenyeviti wa Bunge watatu waliomsaidia kwa karibu sana. Watanzania kwa kawaida huwa wanasahau historia haraka, lakini Wenyeviti hao wa Bunge waliomsaidia Mzee Sitta kufanikisha Bunge la Tisa ni mimi mwenyewe niliyesimama hapa, ni Mheshimiwa Jenista Mhagama ambaye sasa ni Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu, lakini pia na Mheshimiwa Zubeir Maulid, ambaye leo ni Spika wa Bunge la Zanzibar. Mnaweza mkaona ninyi wenyewe ni jinsi gani ambavyo mzee alikuwa ana uwezo wa kulea na matokeo ya ulezi wake ni nini. *(Makofi)*

Kama nilivyosema, Mzee Samuel Sitta alikuwa ni mwana mageuzi, mboreshaji ambapo pia katika sifa hizo najisikia fahari kwa fursa alizonipa ili kumsaidia vizuri katika Bunge hilo la Tisa kama nilivyosema. Pia tukumbuke kwamba Mzee Sitta alirithi Kanuni ambazo aliona itafaa sana iwapo zitaboreshwa ili kuakisi mfumo wa Kibunge wa Jumuiya ya Madola bila kuathiri mila na tamaduni zetu. Hivyo, aliunda timu ya Wabunge ili kupitia upya Kanuni zetu mwaka 2006. *(Makofi)*

Alinipa heshima kubwa ya kuwa Mwenyekiti wa Kamati hiyo ya kuhuisha Kanuni zetu. Mwenyewe Mzee Sitta akiita Kamati ya Ndugai, ambayo ilikuwa pia na Waheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe ambaye sasa ni Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Nimrod Mkono, marehemu Mheshimiwa Beatrice Shelukindo na marehemu Mheshimiwa Janguo aliyekuwa Mbunge wa Kisarawe wakati huo. *(Makofi)*

Timu hii ndogo ilifanya kazi kubwa sana ya kutoa Kanuni ambazo leo tunazitumia. Yalikuwa ni mabadiliko makubwa sana kutoka Kanuni za zamani ambazo kwa kweli kwa kiasi kikubwa zilikuwa zimeshapitwa na wakati. Miongoni mwa mambo mapya yaliyotokana na Kanuni hizo tulizozifanyia kazi ni pamoja na sasa mnapoona tunaimba Wimbo wa Taifa nyakati za kuanza na kuahirisha Bunge au kama leo tulivyofanya. Kabla ya Mzee Sitta wakati huo hakuna wakati Wimbo wa Taifa uliwahi kuimbwa ndani ya Bunge. *(Makofi)*

Pia katika mabadiliko hayo, ndipo kilipoanza kipindi cha maswali ya papo kwa papo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kabla yake kipindi kama hicho hakikuwepo kabisa. *(Makofi)*

Vilevile wakati huo wa mabadiliko hayo, ndiyo kwa mara ya kwanza tumekuwa na Kamati za Fedha zenye kuongozwa na wajumbe kwa nafasi ya Mwenyekiti kutoka Vyama vya Upinzani ili kuboresha uwajibikaji kama ilivyo katika Mabunge mengine. Baadhi yetu wanaweza wasikumbuke ni lini mambo haya yamekuwa. *(Makofi)*

Pia ndipo tulipopata nafasi katika Utumishi wa Bunge wa kuwa na mwajiriwa ambaye ni Mshauri wa Sheria wa Masuala ya Bunge na kuwa na Idara Maalum kwa ajili ya kuwasaidia Wabunge katika kujenga hoja au katika kuleta Miswada Binafsi au kufanya mabadiliko yoyote ya sheria ili kusaidia Wabunge kuchambua sheria hizo ndani ya Kamati na hata kwa Mbunge mmoja mmoja. *(Makofi)*

Aidha, kipindi hicho ndipo ilipoanzishwa Ofisi ya Bajeti na Mfuko wa Wabunge Majimboni *(Constituency Development Fund)*. Vilevile limesemwa hapa alikuwa na msisitizo sana wa kuwa na Bunge lenye meno na Bunge huru. *(Makofi)*

Marehemu Mzee Sitta alifanya mambo mengi, muda wa leo hautoshi tu kuyaeleza yote makubwa na madogo. Kwa mfano, katika madogo lakini ni muhimu, wakati huo kabla ya Mzee Sitta aliyekuwa anavaa joho humu Bungeni alikuwa ni Spika peke yake. Alipokuja Mzee Sitta akafanya mabadiliko na kuanzia wakati huo Naibu Spika akavaa joho, Wenyeviti wa Bunge wakavaa majoho, Makatibu hapa Mezani mnawaona wana majoho; ni sehemu ya mabadiliko ambayo yalifanyika katika kipindi chake. Kwa mtu mbinafsi

asingefanya hivyo, angebakia yeye na marembo haya, wenzake hawana. *(Makofi)*

Namkumbuka Mzee Sitta mwaka 2011, alinipigania sana kwenye Mkutano wa Jumuiya ya Madola uliofanyika Kuala Lumpur - Malaysia mpaka nikachaguliwa na Mkutano ule wa Kimataifa wa Jumiya ya Madola, mimi Job Ndugai kuingia katika Kamati ya Utendaji ya Jumuiya ya Madola ya Dunia ambayo Makao yake Makuu ni London na nikawa Mjumbe wa Kamati hiyo ya Utendaji kwa miaka mitatu, nikikutana na Maspika wa nchi mbalimbali katika vikao vya kila miezi mitatu, miezi minne, Maspika wa kuanzia Canada mpaka Australia pamoja na Afrika. Pia kwa nafasi hiyo nikawa Mjumbe wa Kamati ya Utendaji ya Mabunge ya *Commonwealth Africa,* nikikutana na Maspika wa kuanzia Afrika ya Kusini, Nigeria, Ghana, Sierra Leone na kadhalika katika nchi zinazoongea Kiingereza. Sikujua Mzee Sitta alikuwa ameona vipawa gani ndani yangu na ndiyo maana leo hii mnaona nimesimama hapa, niko imara. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nimepokea salamu za rambirambi kwa niaba yenu kutoka kwa viongozi mbalimbali; kwa kifupi nitoe za wachache. Kwanza, kwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Pia nimepokea salamu kutoka kwa Mheshimiwa Dkta.Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Daniel Kidega ambaye ni Spika wa Bunge la Afrika Mashariki ameleta salamu zilizowasilishwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Adam Kimbisa ambaye ni Mbunge wa Afrika Mashariki na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Dodoma. *(Makofi)*

Pia nimepokea salamu kutoka kwa Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar; Mheshimiwa Salim Ahmed Salim, Waziri Mkuu Mstaafu; Jenerali Davis Mwamunyange, Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama; Mheshimiwa Mathias Chikawe, Balozi wa Tanzania nchini Japan; Mheshimiwa Wilson Masilingi, Balozi wa Tanzania nchini Marekani; Kamishna Jenerali Casmir Minja wa Jeshi la Magereza; Mheshimiwa John Magale Shibuda, Katibu Mkuu wa Chama cha *TADEA* na salamu nyingine nyingi kutoka kwa Mabunge mbalimbali duniani. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba hivi karibuni binafsi niliugua sana, kwa akili ya kawaida ya mwanadamu nilikwishakata tamaa na kila siku najiuliza kwa nini Mwenyezi Mungu alinirudisha, majibu ya swali hili mpaka leo sina. Nisimame hapa kumshukuru sana Mzee Sitta na kusema kwamba katika maombi yangu kwa Mwenyezi Mungu ni kwamba aniwezeshe na mimi nitende angalau sehemu tu ya aliyoyafanya Mzee Sitta kwa Bunge hili. *(Makofi)*

Kwa jinsi hiyo, kwa niaba yenu natoa pole nyingi sana kwa mwenzetu, Mheshimiwa Mama Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo, Mjane wa marehemu, watoto, familia, wananchi wa Urambo na Watanzania wote kwa ujumla kwa msiba huu mkubwa na tunamuomba Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tuendelee. Katibu!

NDG. NENELWA M. WANKANGA – KATIBU MEZANI: Maelezo ya utaratibu wa kutoa heshima za mwisho na kusindikiza mwili wa Marehemu.

SPIKA: Naomba utaratibu huo utolewe na Katibu wa Bunge.

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE: Waheshimiwa Wabunge, naomba niende haraka kidogo kwa sababu ya muda. Mara baada ya kikao hiki maalum kukamilika, utaratibu wa kutoka ukumbini na kutoa heshima za mwisho utakuwa kama ifuatavyo:-

Mwili wa Marehemu utatolewa ukumbini na Mpambe wa Bunge na kufuatiwa na familia na ndugu wa marehemu waliopo ndani ya ukumbi huu ambao wataelekezwa sehemu ya kukaa karibu na eneo utakapowekwa mwili.

Kikao cha Bunge cha kawaida kitaendelea ambapo Spika atawahoji Wabunge kuhusu Hoja ya Kuahirisha Bunge itakayotolewa na Mheshimiwa Waziri Mkuu ili aliahirishe Bunge na baadaye Wimbo wa Taifa utaimbwa. Baada ya Bunge kuahirishwa, msafara wa Spika utatoka ukumbini na baadaye Waziri Mkuu na Kiongozi wa Upinzani Bungeni nao watafuata wakisindikizwa na *Sergeant at Arms*. Waheshimiwa Wabunge wote mnaombwa kuendelea kubaki katika viti vyenu mpaka mtakapoelekezwa utaratibu mwingine wa kufanya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kutoka chumba cha kubadilisha nguo, ataungana na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mkuu wa Mkoa, Mzee atakayewakilisha Wazee wa Mkoa wa Dodoma na Katibu wa Bunge kwa niaba ya watumishi wataweka mashada ya maua katika jeneza la Marehemu Mzee Samuel John Sitta.

Baada ya hapo, Wabunge na Viongozi wa Kitaifa waliopo kwenye Jukwaa la Spika wataanza kutoka na kupita eneo ulipowekwa mwili kwa ajili ya kutoa heshima za mwisho kisha watatoka nje ya ukumbi.

Waheshimiwa Wabunge wanaopenda kusindikiza mwili wa marehemu uwanja wa ndege mnaombwa baada tu ya kupita pembeni ya jeneza kwa maana ya kulia na kushoto mwa jeneza ambalo litakuwa mara tu baada ya

lango kuu, mnaombwa muelekee uwanja wa ndege kwa ajili ya kuupokea mwili.

Baada ya zoezi hilo la kutoa heshima za mwisho kukamilika, mwili utatolewa nje na Mpambe wa Bunge na kufuatiwa na wanafamilia kuelekea uwanja wa ndege tayari kwa safari ya kwenda Urambo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Ahsante sana Katibu wa Bunge. Katibu!

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE: Mwili wa Marehemu kutolewa ukumbini na kuwekwa sehemu iliyoandaliwa kwa ajili ya heshima za mwisho.

SPIKA: Sasa naomba *Sergeant at Arms* muingie kwa ajili ya kuutoa mwili wa Marehemu na mwili utakapokuwa unatoka tutamuomba Mheshimiwa Mama Margaret Sitta na familia pia mtaambatana na jeneza.

Sergeant at Arms naomba mharakishe, muda hauko upande wetu, mnaruhusiwa kuingia sasa na hatua zote zitakazofuata tujitahidi kwenda kwa kuokoa muda.

Waheshimiwa Wabunge, sasa naomba tusimame.

MWILI WA MAREHEMU KUTOLEWA UKUMBINI

(Hapa Mwili wa Marehemu spika Mstaafu
Mzee Samuel John Sitta Ulitolewa Ukumbini)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Katibu!

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:

HOJA YA KUAHIRISHA BUNGE

SPIKA: Hoja ya Kuahirisha Bunge, naomba nimuite Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

WAZIRI MKUU: Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kutoa pole kwako, Waheshimiwa Wabunge wote na Watanzania kwa ujumla kwa kupata msiba wa mzee wetu Mheshimiwa Samuel Sitta, Mbunge Mstaafu wa Jimbo la Urambo, Mkoani Tabora, Spika Mstaafu wa Bunge la Tisa toka mwaka 2005 mpaka 2010 na Mwenyekiti wa Bunge Maalum la Katiba na Kiongozi

aliyetumikia Taifa katika nyadhifa mbalimbali. Pia nikupe pole kwa msiba wa mzee wetu Joseph Mungai, Mbunge Mstaafu na Waziri katika Serikali za Awamu zilizopita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukiwa kwenye majonzi ya kuuaga mwili wa Mheshimiwa Samuel Sitta hapa ndani, Spika Mstaafu, kwa mshtuko na masikitiko, leo alfajiri tulipokea taarifa ya msiba wa Mbunge mwenzetu, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir, Mbunge wa Dimani, Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, Marehemu Hafidh Ali Tahir amekuwa mwakilishi mzuri wa wananchi wa Dimani, mwenzetu hapa Bungeni, mwanamichezo, *referee* wa Kimataifa chini ya *FIFA,* Mtangazaji wa Shirika la Utangazaji Zanzibar, Mshauri wa michezo wa aliyekuwa Rais wa Zanzibar, Dkt. Salmin Amour. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kuwa Mheshimiwa Hafidh Tahir tumeshirikiana naye katika shughuli mbalimbali za Bunge na michezo mpaka siku ya jana usiku. Ni usiku wa kuamkia leo alipopata tatizo la afya, aliamua kwenda hospitali yeye mwenyewe akiendesha gari usiku ule na akiwa hospitali hali ilibadilika na hatimaye kuaga dunia. Ni tukio la kusikitisha sana. Mwenyezi Mungu azilaze roho za Marehemu hawa wote mahali pema peponi.

Mheshimiwa Spika, kwa majonzi makubwa, naomba kutumia nafasi hii pia kutoa pole sana kwako wewe binafsi, Waheshimiwa Wabunge wenzangu na Watanzania kwa ujumla.

Aidha, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, leo hii nilitakiwa kutoa hotuba ya kuahirisha Mkutano wa Tano wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuisoma hapa mbele yenu. Katika mazingira haya sitaweza kusoma hotuba yangu, naomba sana itoshe na iridhiwe nanyi kuwa hotuba hii iingie katika *Hansard* na kuwekwa katika tovuti ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na tovuti nyingine zote za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa makofi haya, inaashiria kwamba Waheshimiwa Wabunge mmeridhia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, baada ya maelezo haya ninaomba kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu sasa liahirishwe hadi tarehe 31Januari, 2017, siku ya Jumanne saa tatu asubuhi, litakapokutana tena katika ukumbi huu hapa Dodoma. Mwenyezi Mungu awapokee miongoni mwa wema.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Mheshimiwa Spika, samahani, naomba nirudie tena, na naomba irekebishwe pia.

Mheshimiwa Spika, kwa maana hiyo baada ya maelezo haya ninaomba kutoa hoja kuwa Bunge lako Tukufu sasa liahirishwe hadi tarehe 31 Januari, 2017 siku ya Jumanne saa tatu asubuhi, litakapokutana tena ndani ya ukumbi huu hapa Dodoma. Mwenyezi Mungu awapokee miongoni mwa wema.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Bunge liliridhia kuahirishwa Bunge mpaka Tarehe 31 Januari, 2017, Saa Tatu Asubuhi, Mjini Dodoma)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

HOTUBA YA MHESHIMIWA KASSIM M. MAJALIWA (MB), WAZIRI MKUU WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WAKATI WA KUAHIRISHA MKUTANO WA TANO WA BUNGE LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA TAREHE 11 NOVEMBA, 2016 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

UTANGULIZI

1. Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutulinda na kutufikisha salama siku ya leo tunapohitimisha Mkutano wa Tano wa Bunge lako Tukufu tuliouanza tarehe 1 Novemba, 2016.

2. Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii pia kukupa pole, kwa msiba mzito uliotokea tarehe 7 Novemba, 2016 ambao Bunge lako tukufu, Serikali na Taifa tumepata kwa kumpoteza Mheshimiwa Samwel Sitta, mmoja wa Viongozi mahiri wa Bunge hili katika historia ya nchi yetu. Msiba uliotupata wa aliyekuwa Spika Mstaafu wa Bunge la Tisa (2005-2010) na Mbunge Mstaafu wa Jimbo la Urambo Mkoani Tabora ni pigo kwa Taifa letu. Nasi Wabunge kwa kuwawakilisha Watanzania leo hii muda mfupi ujao tutaaga mwili wa kipenzi chetu Mheshimiwa Samuel Sitta. Tunamwomba **Mwenyezi Mungu ailaze Roho ya Marehemu mahali pema Peponi. Amina.**

3. Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kutoa pole kwa mjane wa marehemu, Mheshimiwa Margareth Simwanza Sitta, Mbunge mwenzetu, watoto wake na wanafamilia wote na marafiki wote kwa ujumla kutokana na msiba mzito uliowapata. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awape subira katika kipindi hiki kigumu cha majonzi na siku zote wamtangulize Mwenyezi Mungu katika kuwaongoza wanafamilia waliobakia.

Sina budi kukiri kuwa Taifa limempoteza mtu muhimu aliyetoa mchango mkubwa katika uongozi na maendeleo. Enzi za uhai wake, Marehemu Mheshimiwa Sitta, alibahatika kufanya kazi na Marais wa awamu zote nne zilizopita tangu ya kwanza ya Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, akiwa Mbunge kwa miaka 30. Alikuwa ni Spika wa Bunge la Tisa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Nyadhifa nyingine alizowahi kushika ni pamoja na Mkuu wa Mikoa ya Iringa na Kilimanjaro, Waziri wa Ujenzi, Waziri aliyesimamia Ustawishaji Makao Makuu, Waziri wa Katiba na Sheria, Waziri wa Afrika Mashariki, Waziri wa Uchukuzi na Mwenyekiti wa Bunge Maalumu la Katiba.

4. Mheshimiwa Spika, tarehe 8 Novemba, 2016 tumeondokewa tena na Kiongozi wa muda mrefu Serikalini Ndugu Joseph Mungai. Kiongozi huyu ameshika nafasi mbalimbali katika utumishi wa umma ikiwemo Ubunge na Uwaziri.

5. Mheshimiwa Spika, tangu tulipokutana mara ya mwisho, pametokea majanga mbalimbali yakiwemo maradhi, ajali, na matukio mengine ambayo yamesababisha vifo na majeruhi kwa Watanzania wenzetu. Sote tunakumbuka tukio la kusikitisha la watumishi wa Serikali waliopoteza maisha wakiwa kazini walipovamiwa na wanakijiji wa Makang'wa wilayani Chamwino mkoani Dodoma. Nalaani mauaji hayo na kuvitaka vyombo vya usalama kuwachukulia hatua wote waliohusika. Vilevile, katika miezi ya Oktoba na Novemba, kumetokea ajali za barabarani katika Mikoa ya Mbeya, Pwani, Singida, Lindi, Iringa, na ile iliyopoteza ndugu zetu 19 mkoani Shinyanga na kwingineko ambako ndugu zetu walipoteza maisha. Ninatoa pole kwa wafiwa wote na wale wote waliopatwa na majanga kutokana na matukio hayo. Tunawaombea afya njema wale waliopata majeraha na waliopo hospitali. Pia niendelee kuwataka Askari wa usalama barabarani kuhakikisha wanasimamia madereva na watumiaji wa Barabara kuzingatia Sheria za usalama wa barabarani.

6. Mheshimiwa Spika, leo tunahitimisha Mkutano huu wa Tano tukiwa tumekamilisha shughuli zote zilizopangwa. Naomba nitumie fursa hii kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kukamilisha kazi zote kwa ufanisi mkubwa. **Nawapongeza sana!**

SHUGHULI ZA BUNGE

7. Mheshimiwa Spika, katika mkutano huu tumepata fursa ya kujadili, kupokea na kushauri kuhusu mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa unaokusudiwa kutekelezwa na Serikali pamoja na muongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Aidha, katika kipindi hiki, tumejadili Hoja mbalimbali za Serikali ikiwemo Miswada, Taarifa za Kamati, Mkataba wa EPA, Maazimio na Kauli mbalimbali za Mawaziri. Vilevile, Wabunge walipata majibu ya maswali mbalimbali ya msingi na ya nyongeza yaliyoulizwa na Waheshimiwa Wabunge na maswali ya Papo kwa Papo kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

8. Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Mwanasheria Mkuu wa Serikali, pamoja na Wataalam wake, kwa kazi kubwa ya kuandaa miswada mbalimbali iliyowasilishwa katika Bunge lako Tukufu. Aidha, napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri. Serikali itazingatia ushauri na maoni yenu wakati wa utekelezaji.

MAAZIMIO

9. Mheshimiwa Spika, katika mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kupokea na kujadili Mkataba wa Ubia wa Uchumi baina ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Umoja wa Ulaya yaani *East Africa Community – European Union Economic Partnership Agreement*. Napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu mizuri tuliyoipata wakati wa mjadala wa Mkataba huo. Serikali itafanyia kazi maoni, ushauri na uamuzi wenu kuhusu Mkataba huo.

JUHUDI ZA SERIKALI ZA KUWAHUDUMIA WAATHIRIKA WA TETEMEKO LA ARDHI MKOANI KAGERA

10. Mheshimiwa Spika, mtakumbuka kuwa mnamo tarehe **10 Septemba, 2016** lilitokea tetemeko la ardhi katika eneo la Kanda ya Ziwa na hususan Mkoa wa Kagera. Tetemeko hilo lilisababisha athari mbalimbali zikiwemo vifo, majeruhi, uharibifu wa makazi na miundombinu ya umma na watu binafsi. Jumla ya Watu **117,721** wameathirika kwa kupoteza makazi yao, mali na athari za kisaikolojia katika Wilaya za Bukoba, Missenyi, Muleba, Karagwe na Kyerwa. Aidha, jumla ya watu **17** walipoteza maisha na **560** walijeruhiwa. Vilevile, nyumba 2,072 za makazi zilianguka kabisa na nyumba 14,595 za makazi zilibomoka, baadhi zina kuta au kupata nyufa kubwa na hivyo kuzifanya kuwa hatarishi kwa makazi ya binadamu. Vilevile, maafa haya yalisababisha uharibifu wa miundombinu ya barabara na majengo ya Serikali 1,718 yaliyoharibika kwa viwango tofauti.

11. Mheshimiwa Spika, kufuatia hali hiyo, Serikali ilianzisha **Kituo cha Operesheni na Kuratibu Maafa** kwenye Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kagera kwa lengo la kuharakisha huduma. Aidha, Serikali ilitoa matibabu bure kwa majeruhi wote, kuandaa na kugharamia mazishi ya watu **17** waliofariki ambapo **mimi binafsi nilihudhuria na pia kutoa mkono wa pole wa Shilingi Milioni 17 kwa wafiwa.** Vilevile, Serikali kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali iliwahudumia wananchi walioathirika na tetemeko kwa kuwapatia misaada ya kibinadamu ikiwemo chakula, madawa, nguo, makazi ya muda, vifaa vya ujenzi, vifaa tiba, vifaa vya shule na huduma ya ushauri wa kisaikolojia. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwakilishi Mkazi wa Umoja wa Mataifa na wadau mbalimbali walifanya Tathmini ya pamoja ya mahitaji ya haraka katika kukabiliana na Athari za Tetemeko hilo. Ambapo utekelezaji wa masuala muhimu yaliyoainishwa katika tathmini hiyo unaendelea.

12. Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha wadau, taasisi na wananchi mbalimbali kuchangia maafa hayo, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na **Kamati ya Maafa** ya Mkoa wa Kagera ilifungua **Akaunti pekee Namba 0152225617300 katika Benki ya CRDB Bukoba yenye** jina la **"KAMATI MAAFA KAGERA"**. Hadi kufikia tarehe **10 Novemba, 2016** kiasi cha Shilingi **5,427,671,677.32 kilikuwa kimeingizwa kwenye Akaunti hiyo. Hadi kufikia tarehe 10 Novemba 2016 Salio katika Benki ni Shilingi 4,296,038,711.79 na matumizi hadi tarehe tajwa yalikuwa ni Shilingi 1,130,428,347.53**. Aidha, Kamati pia ilisajili namba za simu za mkononi za kupokea michango katika Kampuni za Vodacom (**M-Pesa) 0768 196 669,** Tigo (**Tigopesa) 0718 069 616** na Airtel **(Airtel Money) 0682 950 009** kwa jina la **"KAMATI MAAFA KAGERA"**. Hadi kufikia tarehe **10 Novemba, 2016,** kiasi cha **Shilingi 16,638,747** kilichangwa kupitia mitandao hiyo ya simu. Hivyo kufanya jumla ya fedha zilizopokelewa kupitia Benki na Mitandao ya Simu kuwa **Shilingi 5,444,310,424.32.** Aidha, Serikali imechangia **Shilingi Billioni Moja** katika kukabili janga hilo.

13. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kupokea misaada kutoka kwa Washirika wetu wa Maendeleo, Balozi na hata Nchi marafiki. Mathalan, tumepokea kutoka Serikali ya Uganda **Dola za Kimarekani 200,000** sawa na **Shilingi Milioni 419.2**, Serikali ya India **Shilingi Milioni 547**, Serikali ya Kuwait **Shilingi Milioni 51** na Serikali ya Uingereza iliahidi kutoa **Shilingi Bilioni Sita** zitakazoelekezwa kwenye ujenzi wa shule.

14. Mheshimiwa Spika, tumepokea vifaa mbalimbali vyenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 357 yakiwemo maturubai, magodoro, ndoo, mashuka, vifaa tiba, dawa na chakula kutoka Serikali za Japan, China, Kenya, Pakistan, Burundi na Rwanda.

15. Mheshimiwa Spika, taarifa ya Kikosi Kazi cha Wataalam imeainisha kuwa takribani Shilingi **Bilioni 63.2** zitahitajika kurejesha hali ya kawaida katika Mkoa

wa Kagera kufuatia maafa hayo. Gharama hii inajumuisha ukarabati wa shule za msingi, sekondari, vituo vya afya na taasisi nyingine katika wilaya zote sita za Mkoa huo, ujenzi mpya wa shule za Ihungo na Nyakato (tayari wafadhili wamejitolea kujenga shule hizi). Aidha, hadi kufikia tarehe **10 Novemba, 2016** kiasi cha Shilingi **966,898,826** zilitumika katika kufanya ukarabati mkubwa na mdogo wa Shule za Msingi na Sekondari pamoja na Zahanati katika Halmashauri za Mkoa wa Kagera. Serikali inaendelea na ujenzi wa Zahanati mpya (Ishozi) inayojumuisha chumba cha Upasuaji na wodi ya kinamama na watoto na usimamizi wa ujenzi wa shule za Ihungo na Nyakato. Aidha, katika kuongeza nguvu ya urejeshaji hali jumla ya Askari 96 wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania wakiwemo Wahandisi, Mafundi, Wapishi, na Madereva waliwasili Mkoani Kagera tarehe **19 Oktoba, 2016** kushiriki katika zoezi la kurejesha hali ya majengo na miundombinu.

16. Mheshimiwa Spika, Serikali inapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu na wananchi kwa jumla kuwa Serikali ipo pamoja na waathirika hawa katika suala hili na ina mikakati madhubuti ya kuhakikisha tunarejesha hali bora kwa kuendelea kurudisha miundombinu, kutoa huduma za kibinadamu na matibabu kwa waathirika. Aidha, napenda kuwashukuru wale wote waliochangia katika kusaidia wenzetu wa Kagera, kwani katika kipindi hiki, tumeonesha umoja wetu, upendo wa dhati, hali ya kuthaminiana na kujaliana. Mungu awabariki sana na kuwaongezea pale walipotoa. Kipekee, niwashukuru Nchi marafiki, Balozi, Wadau wa Maendeleo wa ndani na nje ya Nchi, Taasisi za Kiserikali na zisizo za Kiserikali, Taasisi za Fedha, Kampuni, Vikundi mbalimbali, pamoja na Wananchi wote wakiwemo wale waishio nje ya Nchi.

MAPENDEKEZO YA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2017/2018

17. Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu wa tano wa Bunge, Serikali imewasilisha mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2017/2018. Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa michango yao mizuri iliyotolewa wakati wa kujadili Hoja hiyo. Maoni na ushauri uliotolewa utazingatiwa wakati wa maandalizi ya Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha wa 2017/2018.

TAARIFA ZA KAMATI ZA KUDUMU ZA BUNGE ZA PAC NA LAAC KUHUSU HESABU ZILIZOKAGULIWA KWA MWAKA 2013/2014 NA 2014/2015

18. Mheshimiwa Spika, katika Mkutano huu, Waheshimiwa Wabunge wamepata fursa ya kujadili Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Taarifa za Kamati za Kudumu za Bunge za PAC na LAAC kuhusu Hesabu za Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Serikali za Mitaa zilizokaguliwa kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2014 na tarehe 30 Juni, 2015. Serikali imepokea michango na Hoja za Waheshimiwa Wabunge na itazifanyia kazi.

19. Mheshimiwa Spika, napenda kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge kwamba kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 hadi 2016, Serikali imetakiwa kuchukua hatua kali na za haraka kwa wale wote watakaobainika kujihusisha na ubadhirifu na wizi wa mali ya umma, ukiukaji wa maadili ya Utumishi wa Umma na wale wanaoendeleza vitendo vya rushwa na matumizi mabaya ya fedha za Umma. Kutokana na maelekezo hayo, Serikali ya Awamu ya Tano imeendelea kuimarisha udhibiti wa matumizi ya Serikali na kuchukua hatua kwa Watumishi wa Umma wasiozingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za matumizi ya Fedha za Umma. Maafisa Masuuli wote wanakumbushwa kuzingatia kikamilifu Sheria ya Ununuzi wa Umma na Kanuni zake. Aidha, Maafisa Masuuli wote wanatakiwa kuchukua hatua stahiki za kinidhamu na kisheria kwa Wakuu wa Idara, Vitengo na Taasisi za Serikali wanaofanya malipo yenye mashaka wakati wa kufanya manunuzi ya Umma au kuingia Mikataba na Zabuni tata za utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hatua hizo zitapunguza na kuondoa Hoja za ukaguzi na kuimarisha usimamizi wa fedha za walipa kodi.

SEKTA YA KILIMO

Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao Katika Msimu wa Mvua za Vuli

20. Mheshimiwa Spika, naomba nitoe taarifa kutoka Mamlaka ya Utabiri wa Hali ya Hewa kuwa, kwa kipindi cha Oktoba hadi Desemba 2016 imeonesha kuwa katika maeneo mengi ya nchi, mvua zinatarajiwa kuwa chache, kuchelewa kuanza na mahali pengine kunyesha kwa mtawanyiko usioridhisha. Aidha, kwa maeneo yanayopata mvua za vuli zikiwemo Wilaya za Kyerwa, Missenyi na Karagwe, mvua zilipoanza kunyesha zilikuwa chini ya wastani na kusababisha baadhi ya mazao yaliyopandwa kuathirika. Vile vile, taarifa za Mamlaka ya Hali ya Hewa TMA zinaeleza kuwa katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua zinazoanza mwezi Novemba hadi Aprili, mvua zitachelewa na kunyesha chini ya wastani hadi wastani katika maeneo mengi isipokuwa katika baadhi ya maeneo ya Mtwara Lindi na Ruvuma. Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kuwataka wataalam wa kilimo kuhakikisha wananchi katika maeneo yatakayopata mvua kidogo wanawezeshwa kupata mbegu za mazao yanayostahimili ukame na zinazokomaa haraka.

Aidha, niwashauri wakulima kuandaa mashamba yao mapema na kutumia mbegu hizo zinazokomaa mapema na kustahimili ukame. Niwasihi wananchi na wakulima kuendelea kutumia kwa uangalifu na kuhifadhi akiba ya chakula walichovuna au kununua kwa matumizi katika kaya zao. Nitoe wito kwa Sekta binafsi kuendelea kushiriki katika kutoa masoko ya kununua na kuuza mazao katika maeneo yenye ziada na kuyauza katika maeneo yenye uhaba.

Usambazaji wa Pembejeo za Zao laTumbaku

21. Mheshimiwa Spika, ili kuondoa kero ya upatikanaji wa pembejeo kwa zao la tumbaku kwa msimu wa 2016/2017, Serikali imebadili utaratibu kutoka ule uliohusisha zabuni kwa wauzaji wa kati (middlemen) na kuweka utaratibu mpya unaohusisha wazalishaji wa pembejeo kuzisafirisha pembejeo hizo hadi katika Vyama vya Msingi vya Ushirika moja kwa moja kwa **bei ya Dola za Kimarekani 40.45** kwa mfuko wa NPK (ikilinganishwa na Dola za Kimarekani **52.7** za msimu uliopita), na **Dola za Kimarekani 21** pungufu kwa mbolea aina ya Urea na CAN kwa tani moja ukilinganisha uliopita. Hadi sasa wazalishaji wawili wa mbolea za tumbaku (Kampuni ya Yara Tanzania na Rosier) wamechukua jukumu hilo. Napenda kuchukua fursa hii kuvitaka Vyama vya Ushirika kusimamia kikamilifu mpango huu ili wakulima wazalishe kitaalamu na kuongeza tija katika uzalishaji.

SEKTA YA VIWANDA NA UWEKEZAJI

22. Mheshimiwa Spika, mnamo tarehe 17 Oktoba, 2016, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda, Biashara na Uwekezaji alizindua rasmi matokeo ya Sensa ya Uzalishaji Viwandani ya mwaka 2013 iliyofanyika kwa ushirikiano wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS). Zoezi la sensa hii lilitumia taarifa za uzalishaji za viwanda za mwaka, 2013, yaani viwanda vilivyokuwepo mwaka 2013 na vilivyokuwa vinazalisha. Zoezi la ukusanyaji wa taarifa za uzalishaji, za viwanda lilifanyika mwaka 2014 na mwaka 2015 ilikuwa ni kufanya uchambuzi wa kitalaamu na kuandika ripoti.

23. Mheshimiwa Spika, matokeo ya Sensa hiyo yanaonesha kuwa, kufikia mwaka 2013 Tanzania ilikuwa na jumla ya viwanda 49,243 ambapo viwanda vidogo vinavyoajiri mtu 1 – 4 vilikuwa ni Asilimia 85.13, viwanda vidogo vyenye watu 5 - 49 ni Asilimia 14.02, viwanda vya kati vyenye watu 50 - 99 ni Asilimia 0.35 na viwanda vikubwa vyenye watu kuanzia 100 na kuendelea ni Asilimia 0.5. Hivyo, Asilimia 99.15 ya viwanda vyote nchini ni viwanda vidogo.

24. Mheshimiwa Spika, katika utafiti wa mwaka jana ilionekana kuwa mpaka mwezi Oktoba, 2015 kulikuwa na viwanda 52,579. Aidha, kwa kipindi cha mwaka mmoja tu, yaani kuanzia Novemba, 2015 mpaka Oktoba, 2016 jumla ya viwanda vipya **1,843** vimeanzishwa na kufanya jumla ya viwanda vyote nchini kufikia **54,422**. Ni matumaini ya Serikali kuwa kutokana na juhudi za uhamasishaji zinazofanyika, kasi ya uanzishwaji viwanda na hasa viwanda vidogo na vya kati na vikubwa itaongezeka sana.

25. Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara mbalimbali za Kisekta tayari imebainisha maeneo mbalimbali nchini kwa ajili ya kuchochea uwekezaji kama vile kuendeleza eneo la Mji wa Kigamboni na kutenga maeneo maalum ya Uwekezaji katika Mikoa mbalimbali Nchini. Hatua nyingine ni kuboresha

miundombinu kama vile barabara na reli. Mfano mzuri ni ujenzi wa reli yenye urefu wa kilomita 4 katika kiwanda kipya cha KILUA GROUP cha kutengeneza nondo kilichopo Mlandizi, Pwani. Pia, Serikali inaendelea kuimarisha upatikanaji wa umeme wa uhakika. Kwa viwanda ambavyo vipo karibu na bomba la gesi watasaidiwa kuunganishwa na gesi. Vilevile, Serikali, imechukua hatua madhubuti za kuharakisha upatikanaji wa ardhi ambacho ni kivutio muhimu katika kuhamasisha uwekezaji.

Uongezaji Kasi ya Uwekezaji kwenye Sekta ya Viwanda Nchini

26. Mheshimiwa Spika, Serikali imeweka mikakati madhubuti ya kuhakikisha kasi ya uwekezaji kwenye sekta ya viwanda inaongezeka ili ichangie Asilimia 15 ya Pato la Taifa ifikapo mwaka 2020 Ili kutekeleza adhima hiyo hatua zifuatazo zinaendelea kuchukuliwa:-

Kwanza: Kutambua sekta za kipaumbele kwa kuzingatia viwanda vinavyotumia malighafi za ndani, na hususan kwenye sekta za kilimo na maliasili ili kuchochea uzalishaji vijiini na kuongeza ajira; viwanda vinavyotumia malighafi za ndani ambazo si za kilimo kama vile madini na kemikali; na kuweka msukumo kwenye kuanzisha viwanda visivyotumia malighafi za ndani kama vile uunganishaji wa magari na uzalishaji wa vifungashio.

Pili: Kuandaa Mpango mahsusi wa uwekezaji kwenye viwanda kupitia Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. Mpaka sasa, Mifuko ya LAPF, PPF, PSPF, NSSF na GEPF tayari wameainisha miradi ya uzalishaji watakayoanza nayo.

Tatu: Kuhamasisha Sekta Binafsi, ya ndani na nje ya Nchi, kuwekeza kwenye viwanda. Kupitia makongamano ya biashara na uwekezaji nchi mbali mbali zimehamasishwa kuwekeza nchini. Baadhi ya nchi hizo ni China, Oman, Vietnman, Urusi, Morocco n.k.

Nne: Kuingia makubaliano ya ushirikiano na Nchi zingine ili kuongeza uwekezaji. Mpaka sasa Nchi ya China imechagua jimbo la Jiangsu kuleta viwanda nchini na pia kupitia Jukwaa la Ushirkiano la China na Afrika itawezesha ujenzi wa miundombinu ikiwemo Bandari ya Bagamoyo. Aidha, kwa utaratibu huu Serikali tayari imeanza utekelezaji wa mradi wa kuunganisha matrekta 2400 pale TAMCO Kibaha kufuatia ushirikiano na Serikali ya Poland, uunganishaji wa magari wa Kampuni ya Kitanzania ya SIMBA MOTOR kwa ushirikiano na Jeshi (NYUMBU) na Kampuni ya China. Vile vile, India kupitia mradi wake wa kuimarisha uwekezaji Afrika (SITA) inasaidia utekelezaji wa mikakati minne ya kukuza na kuendeleza alizeti, pamba, ngozi na mazao ya jamii ya kunde.

Tano: Kutoa elimu na mwongozo kwa Serikali ngazi ya Mikoa na Wilaya kuendelea kuhamasisha uwekezaji katika maeneo yao. Serikali imegawa Mikoa

katika makundi manane ambayo Watendaji Waandamizi wa Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji watakwenda kuzungumza na wadau ili kuhakikisha viwanda vinasambaa Nchi nzima.

27. Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza jukumu hili mambo muhimu ambayo Mikoa inatakiwa kuzingatia ni pamoja na Mikoa kuweza kubaini fursa walizonazo na kuandaa taswira ya mkoa kutegemeana na fursa walizonazo. Aidha, Mikoa inahimizwa kuhamasisha wananchi juu ya uwekezaji. Vilevile, Viongozi wa Mkoa wanashauriwa kuongeza kasi ya kuhamasisha Mamlaka za Serikali za Mitaa kutenga maeneo na kuhakikisha kuwa wanazingatia katika mipango ya Halmashauri za wilaya ujenzi wa miundombinu wezeshi kwenye maeneo watakayotenga kwa ajili ya uwekezaji.

SEKTA YA ELIMU

Matokeo ya Mitihani ya Darasa la Saba 2016

28. Mheshimiwa Spika, mwezi Oktoba, 2016 Baraza la Mitihani la Taifa lilitangaza matokeo ya Mitihani wa Darasa la Saba kwa mwaka 2016. Taarifa hiyo ilibainisha kuwa katika mtihani huo, kati ya wanafunzi **789,479** waliofanya mtihani, jumla ya wanafunzi **555,291** walifaulu sawa na Asilimia **70.36**. Kati yao wasichana ni **283,751** na wavulana ni **271,540**. Nitumie fursa hii kuwapongeza wanafunzi wote waliofaulu na Shule zote zilizofanya vizuri na hasa wale kumi bora. Napenda kuwaagiza Viongozi wa Mikoa na Halmashauri kuendelea kukamilisha miundombinu ya vyumba vya madarasa na miundo-mbinu mingine ili kuandaa mazingira ya kuwapokea wanafunzi wanaotakiwa kujiunga na kidato cha kwanza mwezi Januari, 2017. Kila Mkoa uweke lengo la kuhakikisha Wanafunzi wote watakaochaguliwa wanajiunga na Sekondari. Serikali kwa upande wake itahakikisha inatoa ruzuku kwa ajili ya mahitaji ya Wanafunzi watakaojiunga na Sekondari.

Mwenendo wa utoaji wa mikopo

29. Mheshimiwa Spika, tangu mwaka **1994** Serikali ilipoanza kutoa mikopo kwa wanafunzi wa Elimu ya Juu, jumla ya kiasi cha **Shilingi Trilioni 2.44** kimekwishatolewa. Jumla ya wanafunzi **324,994** wamenufaika na fedha hizo.

30. Mheshimiwa Spika, katika mwaka **2016/2017** jumla ya wanafunzi **64,441** wamedahiliwa na Tume ya Vyuo Vikuu na orodha yao kuwasilishwa Bodi ya Mikopo ya Elimu Juu. Kama alivyoeleza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 3 Novemba, 2016, wakati akitoa kauli ya Serikali Bungeni kuhusu upangaji na utoaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu, ni kwamba hadi kufikia tarehe **2 Novemba, 2016** jumla ya wanafunzi **25,228** wa mwaka wa kwanza walikuwa wamekwishapewa fedha za mikopo. Kati ya wanafunzi hao, **4,787** ni

Yatima, **127** wenye Ulemavu na **94** ni waliosoma Sekondari kwa Ufadhili wa Taasisi mbalimbali.

31. Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kuwa wanafunzi wote wanaoendelea na masomo, ambao ni wanufaika wa mikopo na vyuo vyao vimewasilisha Bodi ya Mikopo taarifa za matokeo wameendelea kupatiwa mikopo kama ilivyokuwa katika mwaka uliopita wa masomo.

Changamoto Zilizopo za Mkopo na Utatuzi Wake

32. Mheshimiwa Spika, ili kutatua changamoto zinazojitokeza katika uratibu wa mikopo ya wanafunzi, Serikali inafanya mapitio ya mfumo wa udahili wa wanafunzi vyuoni, utaratibu mzima wa utoaji na urejeshwaji mikopo kwa lengo la kuwa na mfumo bora zaidi na kuondoa adha inayowapata wanafunzi wanapofungua vyuo kutokana na mfumo uliopo sasa. Nimeagiza kazi hii ikamilike mapema ili mapendekezo ya mfumo utakaokuwa na tija zaidi yaweze kuzingatiwa wakati wa maandalizi ya Bajeti ya 2017/2018.

SEKTA YA ARDHI

Hali ya Migogoro baina ya Watumiaji wa Ardhi Nchini:

33. Mheshimiwa Spika, nchi yetu imeendelea kukumbwa na migogoro mbalimbali ya ardhi baina ya watumiaji wa ardhi ikiwemo migogoro mikubwa baina ya wakulima na wafugaji; migororo baina ya wananchi na wawekezaji; wafugaji na hifadhi za Taifa na baina ya wakulima na baadhi ya maeneo ya hifadhi za Wilaya mbalimbali.

Juhudi na Mikakati ya Serikali ya Kuondoa Migogoro Mikubwa ya Wakulima na Wafugaji

34. Mheshimiwa Spika, migogoro ya matumizi ya ardhi baina ya Wakulima na Wafugaji imeendelea kuongezeka kutokana na ongezeko la watu na mifugo, na vijiji kutokuwa na Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi inayoainisha maeneo mahsusi kwa ajili ya Kilimo na Ufugaji. Aidha, uwepo wa mabadiliko ya tabia nchi yanayosababisha ukame na ukosefu wa malisho na maji katika maeneo ya wafugaji kumesababisha uhusiano hafifu baina ya jamii za wafugaji na wakulima kutokana na mifugo kuingizwa katika mashamba ya wakulima kwa mabavu.

35. Mheshimiwa Spika, migogoro hii imesababisha kuwepo kwa vitendo vingi vya uvunjifu wa amani, upotevu wa maisha ya wananchi, baadhi ya wananchi kupata vilema vya maisha, uharibifu wa mali, uharibifu wa mazingira, athari za kijamii kama watoto kushindwa kwenda shule na wananchi kushindwa kushiriki

katika shughuli za maendeleo kutokana na hofu jambo linaloweza kusababisha njaa na umaskini miongoni mwa jamii na Taifa.

Hatua za kutatua migogoro mikubwa ya wakulima na wafugaji

36. Mheshimiwa Spika, ili kukabiliana na migogoro na kuwawezesha wakulima na wafugaji kuendelea na shughuli zao bila migogoro, Serikali inaendelea kutekeleza mikakati ya kuainisha, kupima, kutenga na kumilikisha ardhi kwa ajili ya wafugaji na wakulima; na kanda za malisho kwa wafugaji wakubwa na wadogo itakayohusisha vijiji, Wilaya na Mikoa. Maeneo haya yatakayotengwa yatalindwa kwa kuyatangaza kwenye Gazeti la Serikali, na matumizi yake yatasimamiwa ili kuhakikisha wanafuga kwa kuzingatia uwiano wa malisho na mifugo.

37. Mheshimiwa Spika, mikakati hiyo ni pamoja na kuzigawanya Ranchi zilizopo katika vitalu ili wafugaji wenye ng'ombe zaidi ya 200 wahamie huko, kila kitalu kimoja kulingana na uwezo wa kitaalamu wa kulisha idadi maalum ya ng'ombe. Wafugaji wenye mifugo chini ya 200 watagawiwa maeneo katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili yao katika vijiji na watakuwa wanauza mifugo yao katika minada ambapo wafugaji kutoka Ili katika ranchi watafika kununua mifugo hapo. Kwa mikoa ambayo haina Ranchi za Taifa, watatenga maeneo yaliyo wazi kwa ajili ya wafugaji wakubwa.

38. Mheshimiwa Spika, ili kuzuia wafugaji kuhamahama kutafuta maji na huduma nyingine, Serikali kwa kushirikiana na wafugaji itaweka miundombinu ya majosho, mabwawa ya kunyweshea maji, huduma za ugani zikiwemo matibabu, elimu ya kulima malisho, unenepeshaji, uwekaji sahihi wa chapa za ng'ombe n.k.

39. Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua hizo, jawabu la kudumu la migogoro hii ni kuhakikisha kuwa tunawawezesha wafugaji kuvuna na kupunguza mifugo bila kupata hasara, kupitia uwekezaji wa Viwanda vya Kuchakata Nyama na Usindikaji Maziwa ili kuongeza thamani. Wizara husika zikae pamoja na kubuni Mikakati na Mipango ya kuvutia wawekezaji katika eneo hili katika miaka mitatu ijayo kuwe na tofauti.

40. Mheshimiwa Spika, aidha napenda kuzikumbusha Halmashauri za Wilaya kote nchini kuendelea kuweka na kutekeleza mipango madhubuti ya matumizi bora ya ardhi, na wale wenye Benki ya Ardhi wagawe kwa busara kwa wafugaji, wazuie wafugaji wengine wasiendelee kuingiza mifugo katika maeneo ya kilimo na watumie sheria ndogo zilizopo na kama hazipo ziandaliwe na kutumiwa; na ikibidi wahalifu wapelekwe mahakamani. Aidha, niwakumbushe wafugaji wote kufuata sheria na kwamba Serikali haitasita

kuwachukulia hatua wafugaji watakaoingiza mifugo yao katika mashamba ya wakulima kwa makusudi.

SEKTA YA NISHATI

Mradi Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijijini Awamu ya Pili

41. Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa nishati ya umeme, Serikali imeendelea kutoa mkazo katika kutekeleza na miradi mikubwa ya uzalishaji na usafirishaji umeme pamoja na miradi ya kusambaza umeme vijijini. Ili kuhakikisha huduma ya umeme inawafikia wananchi wengi, hususan waishio vijijini, Serikali kupitia REA imeendelea kutekeleza Mradi Kabambe wa Kupeleka Umeme Vijijini Awamu ya Pili tangu mwaka 2014. Mradi huu unatekelezwa katika wilaya zote za Tanzania Bara. Hadi kufikia Oktoba, 2016 ujenzi wa kilometa za njia ya msongo wa Kilovolti (kV) 33 umefikia **Asilimia 95.6**; ujenzi wa kilometa za njia ya Msongo wa **Volti 400** umefikia **Asilimia 89.3;** na ufungaji wa transfoma umefikia **Asilimia 87.2.** Aidha, jumla ya **wateja 146,311** wa awali sawa **na Asilimia 59** ya lengo la **wateja 255,000** wameunganishiwa umeme kupitia mradi huo.

Mradi Kabambe wa Kusambaza Umeme Vijijini Awamu ya Tatu

42. Mheshimiwa Spika, Mradi huu utatekelezwa kwa kipindi cha miaka 5 katika vijiji **7,873** vya wilaya zote za Tanzania Bara. Takriban vijiji **7,697** vitapelekewa umeme wa gridi ya Taifa na vijiji **176** umeme wa nje ya gridi (*Off-grid*). Mpango huu utaongeza wigo wa usambazaji umeme katika maeneo ambayo hayakufikiwa na miradi ya *REA Turnkey Phase I* na *II*. Ili kutekeleza miradi hiyo kwa kasi zaidi, Serikali ya Awamu ya Tano katika bajeti yake ya mwaka 2016/17 iliongeza fedha za kupeleka umeme Vijijini kutoka **Shilingi Bilioni 357.117** zilizotengwa mwaka 2015/16 hadi **Shilingi Bilioni 587.61** mwaka 2016/17. Hadi kufikia mwezi Oktoba, Serikali imetoa jumla ya Shilingi **Bilioni 109.8** kwa ajili ya Mfuko wa Nishati Vijijini kutoka kwenye vyanzo vya fedha za ndani. Kati ya fedha hizo **Shilingi Bilioni 100.4** ni tozo ya mafuta na **Shilingi Bilioni 9.4** ni tozo ya umeme.

43. Mheshimiwa Spika, zabuni za kupata wakandarasi wa kutekeleza mradi huu zilitangazwa tarehe 1 Agosti, 2016. Kwa sasa REA inaendelea na uchambuzi wa zabuni hizo. Taratibu zote za mradi huo zimepangwa kukamilika mwezi Januari, 2017. Natoa rai kwa viongozi mbalimbali wa Serikali wakimemo Waheshimiwa Wabunge kuwahamisha wananchi katika maeneo yao kutumia fursa ya kuunganishiwa umeme wakati wakandarasi wakiwa kwenye maeneo ya miradi. Katika kipindi hicho bei ya kuunganisha umeme ni **Shilingi 27,000** tu kama ilivyotaarifiwa awali katika Bunge hili.

44. Mheshimiwa Spika, Serikali pia imeanzisha Mradi wa Kupanua Wigo wa Upatikanaji wa Umeme Vijijini (*Tanzania Rural Electricity Expansion Project*). Mradi huo utagharamiwa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia wa Dola za Kimarekani milioni 209. Mradi ulizinduliwa tarehe 26 Agosti 2016, katika kijiji cha Kwedikwazu wilayani Handeni Mkoani Tanga na utawezesha kaya takriban 500,000 kupata huduma ya umeme nchini.

SEKTA YA MADINI

Migodi Mikubwa Kuendelea Kulipa Mrabaha

45. Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha kati ya Oktoba, 2015 na Oktoba, 2016 Serikali ilifanya ukaguzi na kuwezesha migodi mikubwa kulipa mrabaha ambapo: Migodi Mikubwa ya Dhahabu ya Biharamulo, Bulyanhulu, Buzwagi, Geita, New Luika na North Mara imelipa kiasi cha **Dola za Kimarekani Milioni 69.4** ikiwa ni Mrabaha, sawa na Shilingi Bilioni 151.4. Vilevile, Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Ngaka umelipa kiasi cha **Dola za Kimarekani 309,836** na Shilingi Milioni 676 ikiwa ni mrabaha. Aidha, Mgodi wa *TanzaniteOne* umelipa mrabaha wa **Dola za Kimarekani 189,731** sawa na Shilingi Milioni 414.

Kuhamasisha Masoko ya Madini ya Vito Nchini

46. Mheshimiwa Spika, Serikali iliandaa mnada wa madini ya vito, hususan tanzanite uliofanyika kuanzia tarehe 9 hadi 12 Agosti, 2016 Jijini Arusha. Katika mnada huo madini yenye thamani ya **Dola za Kimarekani 3,448,050**, sawa na **Shilingi Bilioni 7.56**, yaliuzwa na kuwezesha Serikali kukusanya **Dola za Kimarekani 150,491.06,** sawa na **Shilingi Milioni 331** ikiwa ni mrabaha kutokana na madini yaliyouzwa.

47. Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kusimamia Sekta za Nishati na Madini ili ziweze kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

TAARIFA YA MAKUSANYO YA FEDHA KWENYE HALMASHAURI KWA MWAKA 2016/2017

48. Mheshimiwa Spika, katika Bajeti ya mwaka 2016/2017 Halmashauri ziliidhinishiwa kukusanya mapato ya **Shilingi Bilioni 665.4.** Hadi kufikia Septemba, 2016 Halmashauri zimekusanya **Shilingi Bilioni 114.46**, sawa na Asilimia **17.2** ya makisio. Kiwango hiki cha ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri bado hakiridhishi. Hivyo, naomba nitumie fursa hii kuhimiza Halmashauri zote nchini kuongeza jitihada katika kukusanya mapato ya vyanzo vya ndani. Nazihimiza Halmashauri kutumia mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji mapato na pia

katika maeneo ya kutolea huduma za afya ili kudhibiti upotevu wa mapato. Aidha, naelekeza Mamlaka za Serikali za Mitaa waimarishe mifumo ya udhibiti wa ndani na kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana katika kila huduma au bidhaa inayonunuliwa na Halmashauri. Halmashauri hazina budi kuepuka matumizi ya fedha yasiyo na tija katika shughuli za uendeshaji wa Mamlaka hizo.

49. Mheshimiwa Spika, Halmashauri zote zinaagizwa zifuatilie kwa karibu mapato na matumizi ya fedha zinazopelekwa kwenye shule na kwenye vituo vinavyotoa huduma za afya ikiwemo Hospitali, vituo vya afya na zahanati. Ili kufikia azma hiyo, uwekwe utaratibu madhubuti wa ukaguzi wa mapato na matumizi ya fedha hizo kwa kushirikisha Wakaguzi wa ndani wa Halmashauri.

MAONI NA MAPENDEKEZO KUHUSU TAARIFA YA KAMATI YA BUNGE YA LAAC

50. Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ushauri mzuri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya LAAC kuhusu ukaguzi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka 2013/2014 na 2014/2015, Serikali imeshatoa maelekezo kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa zinatekeleza kwa ukamilifu maelekezo yote ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa na Kamati nyingine ili kuondoa hoja zilizojitokeza katika taarifa ya CAG. Aidha, Halmashauri zinaelekezwa kuimarisha mifumo ya uthibiti wa ndani na kutumia vizuri ushauri unaotolewa na Kamati za Ukaguzi ili kuimarisha uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma.

51. Mheshimiwa Spika, napenda kusisitiza kwamba Halmashauri zote ni lazima zitekeleze vipaumbele vilivyoidhinishwa katika mpango na bajeti kwa mwaka 2016/17 kwa kupanga vema utekelezaji kwa kuzingatia upatikanaji wa fedha. Halmashauri ziendelee kuimarisha usimamizi wa mikataba ili thamani ya fedha za Serikali iweze kupatikana katika miradi na Kandarasi nyingine zilizoingia Mikataba na Halmashauri.

HITIMISHO

52. Mheshimiwa Spika, wakati tunahitimisha mkutano huu leo, napenda nitumie nafasi hii kukushukuru wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kusimamia vizuri na kwa weledi mkubwa vikao vyote vya mkutano huu. Niwashukuru tena Waheshimiwa Wabunge wote kwa michango yenu. Ninashukuru pia Watendaji wa Serikali kwa kuwasaidia Mawaziri na Naibu Mawaziri katika kujibu maswali na hoja mbalimbali za Wabunge. Niwashukuru wanausalama wote kwa kazi yao nzuri. Niwashukuru madereva wote kwa kuwaendesha Mawaziri, Wabunge na Watendaji wote kwa usalama kabisa. Niwashukuru pia wanahabari wote kwa kuihabarisha jamii juu ya mkutano wetu. Kipekee, nimshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas

Kashililah na timu yake kwa kutuwezesha kukamilisha shughuli zote za mkutano huu kwa mafanikio makubwa.

53. Mheshimiwa Spika, mwisho, lakini si kwa umuhimu, nitumie muda huu kumwomba Mwenyezi Mungu awalinde na awaongoze Waheshimiwa Wabunge wote katika safari ya kurejea majumbani kwenu. Aidha, nawatakia kila la kheri na fanaka katika sikukuu zijazo za mwisho wa mwaka na kuwatakia mwaka mpya wa 2017.

54. Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, napenda kutoa hoja kuwa Bunge lako tukufu sasa liahirishwe hadi tarehe **31 Januari, 2017**, siku ya Jumanne, **saa 3:00 asubuhi** litakapokutana katika ukumbi huu hapa Dodoma.

55. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, kwa jinsi hii, naomba nichukue nafasi hii kuwashukuru sana kwa ushirikiano mkubwa ambao mmetupatia mimi na wenzangu wote tuliokuwa hapa mezani. Kipekee nimshukuru sana Naibu Spika, Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson, Mheshimiwa Andrew Chenge, Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mheshimiwa Najma Murtaza Giga walionisaidia kwa karibu sana kuendesha vikao hivi. Pia niwashukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Waheshimiwa Mawaziri, Waheshimiwa Wabunge, kwa jinsi ambavyo tumeshirikiana vizuri katika Mkutano huu wa Tano.

Waheshimiwa Wabunge, niwatakie kila la kheri muendapo na mtakapokuwa mkirudi kwa tarehe iliyotajwa. Niwatakie kila la kheri kwa Chritsmas na mwaka mpya, niwatakie afya njema na muwasalimie wapiga kura wenu. Katibu!

DKT. THOMAS D. KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:

WIMBO WA TAIFA

SPIKA: Naomba wote tusimame kwa Wimbo wa Taifa.

(Hapa Wimbo wa Taifa Uliimbwa)

SPIKA: Ahsante sana. Naomba sasa nitoe tu maelezo machache, yale ambayo Katibu aliyatoa tukiwa tumesimama hivi.

Waheshimiwa Wabunge, ni kwamba nitatoka, nikishatoka nitafuatiwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kiongozi wa Upinzani Bungeni na Naibu Spika.

Waheshimiwa Wabunge mtaendelea kuwa mmekaa na nitawaomba viongozi wa *gallery* ya Spika na ninyi mtaanza kutoka. Tutakapoanza kuaga pale nje wale ambao wanamaliza kuaga na wenye nia ya kwenda uwanja wa ndege watafanya hivyo moja kwa moja kwa ajili ya kuokoa muda. Ninachosisitiza ni suala la muda kwa vile inatakiwa wafike Tabora mapema iwezekanavyo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa jinsi hiyo, naomba sasa niwaage, naahirisha shughuli za Bunge mpaka tarehe 31 Januari, 2017. Ahsanteni sana.

(Saa 10.32 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumanne, Tarehe 31 Januari, 2017, Saa Tatu Asubuhi)